---

### **UFAPANUZI WA SEHEMU YA I**

‘mwendeshaji farasi kurutu’ ni mtu aliye na kibali cha kuendesha farasi kama kurutu.

‘mwanafunzi wa Mtoaji Mafunzo’ ni mwendeshaji farasi aliye na haki ya kupunguziwa uzito kulingana na Kanuni ya 40.

‘joki’ ni mwendeshaji farasi aliyepoteza haki yake ya kupunguziwa uzito kulingana na Kanuni ya 40.

‘mwendeshaji farasi’ ni mtu aliye na leseni au kibali cha kuendesha farasi kulingana na Kanuni hizi.

## **40. Wanafunzi Waendeshaji Farasi na Kupunguziwa Uzito (27/09/17)**

**40.1** Wanafunzi waendeshaji farasi wana haki ya kupunguziwa uzito lakini lazima wakuwe raia wa Kenya na wenye umri wa kati ya miaka 16 (kumi na sita) na 35 (thelathini na tano). Kibali cha kuendesha farasi kama ‘mwanafunzi anaye ruhusa ya kupunguziwa uzito’ chaweza kupatikana baada ya kufikisha miaka 16 (kumi na sita) katika msimu na chaweza kuendelea kulingana na Kanuni 68.2 mpaka mwisho wa msimu ambawo anafikisha miaka 35 (thelathini na tano).

**40.2** Wanafunzi waendeshaji farasi wanaweza kupunguziwa uzito kama ifwatavyo katika mashindano yote (isipokuwa kama watazuiliwa na masharti ya shindano):

- Kilo 5.0 mpaka pale ambapo wameshinda mashindano 10
- Kilo 3.5 mpaka pale ambapo wameshinda mashindano 20
- Kilo 2.0 mpaka pale ambapo wameshinda mashindano 30

**40.3** Wanafunzi waendeshaji farasi hawapoteza au kupunguza madai yao kwenye kipindi cha kikao. Kupoteza au kupunguzwa kwa madai kutawezekana katika kikao kinachofuata.

**40.4** Hakuna kudai kutoka kwa mwaendeshaji farasi kutakubaliwa anapoendelea kushiriki kwa mashindano ikiwa hajashinda mara thelathini baada ya msimu atakaofikisha umri wa miaka 35 (thelathini na tano).

**40.5** Atakapoacha kupunguziwa uzito baada ya kufikisha miaka 35 (thelathini na tano), mwaendeshaji farasi ambaye aliyeruhusiwa kupunguziwa kilo 2.0 hapo mbeleni anaweza kuendelea kushiriki kwa mashindano kama joki aliyehitimu. Vile vile, mwaendeshaji farasi aliyeruhusiwa kupunguziwa kilo 3.5 au kilo 5.0 hapo mbeleni anaweza kuendelea kushiriki kwa mashindano kutumia kibali cha mwanafunzi mwaendeshaji farasi hadi atakapokuwa ameshinda mashindano 20 (ishirini).

## **TR12. Kizuizi cha Umri**

Wasimamizi wa Kuendesha Farasi hawatatoa leseni kwa mwendeshaji farasi yeyote aliye na umri wa zaidi ya miaka 55 (hamsini na tano). (07/11/19)

## **5. KUPIMA UZANI KABLA YA SHINDANO**

---

**96.** Hakuna mtu ataruhusiwa, bila ya ruhusa maalum kutoka kwa Wasimamizi, kuingia kwenye Chumba cha Kupimia, Chumba cha Kubadilishia isipokuwa Ofisa wa kikao, Ofisa aliyeteuliwa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, Mtoaji Mafunzo na mwendeshaji, msaidizi wake au mtu mwingine anayemtunza farasi anayehusika kwenye kikao. Mtu wowote anayekataa kuondoka ataripotiwa kwa Wasimamizi.

### **97. Kupima Uzani Kabla ya Shindano**

**97.1** Hamna mwendeshaji farasi atapimwa uzani wake kabla ya shindano (isipokuwa kama ilivyotajwa hapa chini) katika shindano lolote isipokuwa kama jina la shindano na lile la farasi na mwendeshaji farasi vyote vimetolewa kwa maandishi na kupigwa sahihi na Mmiliki, Mtoaji Mafunzo, au Ajenti Aliyeidhinishwa kikamilifu katika Ofisi ya Usajili.

**97.2** Tangazo la mwisho la waendeshaji farasi litakuwa 11:00 asubuhi Jumatano ama ilivyochapishwa katika karatasi za manjano. Vifaa vyovyote vya kubebwa na mkimbijaji aliyetangazwa isipokuwa vifaa vya kichwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 46 vitakavyobebwa vitatangazwa na mwendeshaji farasi kwenye mizani wakati atakapokuwa akipimwa kwa minajili ya kabla ya shindano. Idadi ya wakimbijaji, pamoja na majina ya waendeshaji farasi na droo ya nafasi husika, vyote vitaonyeshwa kwenye ubao wa nambari za shindano la kwanza haraka itakavyowezekana, na katika mashindano yatakayofuata pindi tu baada ya shindano litakalokuwa limetangulia kufanywa. Baada ya nambari hizo kuonyeshwa, hakutakuwa na nyongeza au mabadiliko yoyote (isipokuwa kama hali hii itaruhusiwa kwenye Kanuni ya 97.3) yatakayofanywa bila ya ruhusa ya Wasimamizi ambao sababu zao za ruhusa kama hiyo zitaripotiwa kwenye Kalenda ya Shindano la Mbio za Farasi. (10/07/19)

**97.3** Iwapo mwendeshaji farasi, ambaye ametangazwa kuendesha farasi hatajiwasilisha ili kuweza kupimwa, mwendeshaji farasi mwingine anaweza kusawazishwa kwa ruhusa Wasimamizi; mradi tu siku zote anaweza kupimwa uzani ndani ya muda ule uliobainishwa katika Kanuni ya 97.4 ya Kanuni hii lakini wasipotosheka, baada ya kuulizia kwamba kutokuwepo kwa mwendeshaji farasi au kuondolewa kwa farasi kulikuwa kutokana na sababu zisingeweza kuepukika, wataweza, baada ya kushughulikia kesi hii kulingana na nguvu zao, kutoa ripoti kuhusu kesi hii kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**97.4** Kila mwendeshaji farasi lazima apimwe uzani kulingana na farasi aliyebainishwa na Karani wa Mizani kwenye sehemu mwafaka, kwenye muda usiopungua dakika 30 (thelathini) kabla ya wakati uliopangiwa shindano kwanza na kwenye muda usiopungua dakika 25 (ishirini na tano) kabla ya wakati uliopangiwa mashindano yaliokuatia. Mara mbili tu ambapo muda wa dakika ishirini na tano hautazingatiwa ni wakati mwendesha farasi aliyeshinda anaendesha farasi katika shindano lifuatalo na wakati mwendesha farasi anafaa kubadilisha tandiko la farasi kati ya mashindano mawili yanayofuatana, ambapo mwendeshaji farasi husika lazima apimwe uzani dakika 20 (ishirini) kabla ya wakati uliopangiwa shindano hilo. (21/11/18)

**97.5** Iwapo mwendeshaji farasi, baada ya kupimwa uzani wa farasi aliyebainishwa, na kabla hajapitia Amri za Mwanzilishi, atazuliwa kwa ajali au ugonjwa dhidi ya kushiriki kwenye shindano, mwendeshaji farasi mwengine anaweza kumsawazisha mradi tu kusiwe na kuchelewa kusikoeleweka.

**97.6** Iwapo mwendeshaji farasi ananua kubeba uzani zaidi, lazima atangaze kiwango hicho, wakati wa kutambuliwa kwa uzani wake kabla ya shindano.

**97.7** Hamna mwendeshaji farasi atakayepimwa uzani kabla ya shindano na kuruhusiwa kubeba zaidi ya kilo 3 (tatu), isipokuwa katika hali zinazokubalika na Wasimamizi, ambao lazima watoe ruhusa saa moja kabla ya muda uliotangazwa wa shindano la kwanza katika siku hiyo. (10/05/19)

**97.8** Pale ambapo hakuna ruhusa iliyotolewa kulingana na Kanuni ya 97.7, mwendeshaji farasi mwenye uzani uliozidi kilo 3 (tatu) wakati wa kutambuliwa uzani wake kabla ya shindano, atakuwa amepatikana na hatia ya kosa na mwendeshaji farasi mwengine atachukua nafasi yake kwenye uzani uliopangiwa au ulio karibu na uzani huo. (10/05/19)

**97.9** Wakati wa kupimwa uzani baada ya shindano, au kabla ya shindano, lazima mwendeshaji farasi aweke kwenye mizani na kujumuisha katika uzani wake kila kitu ambacho farasi atabeba au amebeba isipokuwa kofia ya fuvu, mjeledi, hatamu, pete, jezi zifunikazo kichwa au kizuia macho, kila kitu kinachovaliwa kwenye miguu ya farasi. Waendesha farasi, wakati wanapotambuliwa uzani wao kabla ya shindano, watajiwasilisha kwenye mizani wakiwa wamevalia buti zao wakatazovalia kwenye shindano.

## **R15. Kupima Uzani Kabla ya Shindano**

**R15.1** Waendesha farasi wote, baada ya kupimwa uzani kabla ya shindano, wataweza kuwapatia Watoaji Mafunzo husika matandiko yao ya farasi, au Wasaidizi wao, ambao hawafai kuyaacha matandiko hayo ya farasi vivyohivyo tu.

**R15.2** Matandiko ya farasi hayafai kurudishwa kwenye Chumba cha Kubadilishia Nguo baada ya waendesha farasi kupimwa uzani wao mwanzoni mwa shindano.

## **TR2. Kusawazishwa kwa Waendesha Farasi Waliotangazwa**

**TR2.1** Waendesha farasi waliotangazwa wanaweza kusawazishwa kama yoyote kati ya yafuatayo yanatumika:

**TR2.1.1** Ugonjwa, au mwendeshaji farasi ametangazwa kutofaa kuwa mwendeshaji farasi kulingana na Kanuni ya 97.5.



**TR2.1.2** Mwendeshaji farasi aliyetangazwa hajiwasilishi ili kupimwa uzani kulingana na Kanuni ya 97.3.

**TR2.1.3** Iwapo mwendeshaji farasi wa mwanzo atapatikana kuwa na uzani uliozidi wa kilo 3 (tatu) kulingana na Kanuni ya 97.8. (10/05/19)

**TR2.1.4** Mwendeshaji farasi alitangazwa kuendesha farasi mwengine kutoka kwenye yadi sawa kwenye shindano sawa, naye farasi hawezi kukimbia katika shindano.

**TR2.1.5** Baadhi ya hali nyinginezo zinazokubalika kwa Wasimamizi.

**TR2.2** Ada za kuendesha farasi zinazofaa kulipwa kama ilivyoagiziwa na Wasimamizi.

## **6. KUPIMA UZANI BAADA YA SHINDANO**

---

**113.** Baada tu ya kufikia mwisho wa shindano na kutulia, mwendeshaji farasi mshindi wa kwanza na waendesha farasi washindi wa pili, tatu, nne na tano katika kila shindano lazima waendeshe farasi zao hadi katika sehemu iliyotengwa kwa minajili ya kuondoa matandiko ya farasi. Waendesha farasi wengine wanaweza kushuka kutoka kwenye farasi wao kwenye kitalifa kinachoeleweka. Katika hali ambazo Jaji angali anashauriana na kurejelea picha na bado hajatangaza uamuzi wake kabla ya waendesha farasi kurudi na kupima uzani baada ya shindano, waendesha farasi hao wanaweza kushuka ama ndani ama kwenye kitalifa kinachoeleweka katika sehemu iliyotengwa ya kuyaondoa matandiko ya farasi mshindi. Katika hali kama hizo, Karani wa Mizani ataweza kupima uzani baada ya shindano kwa wale waendesha farasi wote mpaka pale ambapo uamuzi wa Jaji utakapotangazwa. Lazima kila mwendeshaji farasi ajiwasilishe kwa Karani wa Mizani ili kuweza kupimwa mara moja, na kama alishindwa kukamilisha shindano basi aripoti sababu. Iwapo mwendeshaji farasi atazuiliwa kurudi hadi kwa Karani wa Mizani ili kuweza kupimwa kutokana na ajali au ugonjwa, ambapo yeye au farasi wake wamelemazwa, anaweza kutembea au kubebwa hadi kwenye mizani. Kama mwendeshaji farasi ni mgonjwa sana kiasi cha kwamba hawezi kupimwa uzani baada ya shindano, farasi wake hataondolewa kwenye shindano mradi tu kwamba mwendeshaji farasi huyo alipima uzani kabla ya shindano na uzani wake haukupungua uzani wake kamili, na kwamba Wasimamizi wametoshaka kwamba uzani wake kamili ulitumiwa kwenye shindano lote.

**114.** Baada ya waendesha farasi kupimwa uzani wao baada ya shindano na Karani wa Mizani kutosheka na kuonekana kutopungua uzani ambao walipimwa kabla ya shindano, isipokuwa kulingana na Kanuni ya 116, Wasimamizi wataidhinisha ishara kutolewa. Mradi tu hawataidhinisha hali hii mpaka ambapo:

**114.1** Kipindi kinachoruhusiwa kwa minajili ya upingaji kulingana na Kanuni ya 127.4 kimekamilika.

**114.2** Upingaji wowote ambao unaweza kuwa umeandikishwa kwa misingi iliyotajwa katika Kanuni ya 127.4 umeweza kuamuliwa.

**114.3** Uamuzi katika ulizio lolote kulingana na Kanuni ya 129.2 umetolewa. Hakuna upingaji umetolewa kwa misingi yoyote isipokuwa ile iliyotajwa katika Kanuni ya 127.4 utaweza kusikilizwa kabla ya kutolewa kwa ishara.

**114.4** Wasimamizi wamebadilisha uamuzi wa Jaji kulingana na Kanuni ya 29.3.

**114.5** Baada ya ishara kutolewa, hakuna mabadiliko yatafanywa kwenye nambari za mshindi au farasi waliowekwa kwenye bodi.

**115.** Katika kupimwa uzani baada ya shindano mwendeshaji farasi atajumuisha katika uzani wake kila kitu ambacho farasi amebeba kwenye shindano, isipokuwa kama ilivyotajwa katika Kanuni ya 97.9.

#### **116. Uzani Usio Sahihi**

**116.1** Kama mwendeshaji farasi anao uzani ulio zaidi ya kilo 1 (moja) zaidi ya uzani wake kamili ataripotiwa kwa Wasimamizi. Farasi hataondolewa kwenye shindano kulingana na Kanuni hii.

**116.2** Iwapo mwendeshaji farasi hawezi kupata uzani sahihi, Karani wa Mizani atamruhusu nusu kilo zaidi, lakini kama hawezi kupata uzani sahihi, farasi wake ataweza kupitia upingaji kulingana na Kanuni ya 127.4 kuondolewa kwenye shindano na mwendeshaji farasi anaweza kuadhibiwa.

**117.** Iwapo farasi atukuwa na uzani ulio chini kuliko ule anaofaa kuwa nao kulingana na masharti ya shindano na Kanuni hizi, ataweza, kupitia kwa upingaji na kulingana na Kanuni ya 127.4 kuondolewa kwenye shindano.

**118.** Iwapo mwendeshaji farasi hatajiwasilisha ili kupimwa uzani baada ya shindano, au kugusa (isipokuwa bila kukusudia) mtu wowote au kitu chochote isipokuwa mitambo yake mwenyewe kabla ya kupimwa uzani pindi tu anapomaliza shindano au, katika hali ya mshindi wa kwanza, pili, tatu, nne, au tano kushuka kwenye farasi kabla ya kufikia sehemu iliyotengwa kwa kusudio hilo, isipokuwa kama ilivyotajwa kwenye Kanuni ya 113, farasi wake ataweza, kupitia kwa upingaji, kuondolewa kwenye shindano isipokuwa kama anaweza kutosheleza Wasimamizi kwamba alistahili kufanya hivyo kutokana na hali zisizokuwa za kawaida.

#### **R9. Uzani Wote**

Karani wa Mizani ataweza kuwapima waendeshaji farasi wote baada ya shindano katika angaa shindano moja kwa siku bila ya kuwafahamisha waendeshaji farasi hao.

### **7. UTOAJI LESENI KWA WAENDESHAJI FARASI NA KADHALIKA**

---

#### **68. Kuwapatia Leseni Waendeshaji Farasi**

**68.1** Hakuna mtu ataendesha farasi katika shindano lolote mpaka pale ambapo atapata leseni au kibali kutoka kwa Wasimamizi wa Shindano la Mbio za Farasi, isipokuwa kama ilivyotajwa kwenye sehemu za 68.4 na 68.6 za Kanuni hii, na hakuna mtu ataendesha farasi katika shindano lolote kulingana na Kanuni hizi mpaka pale ambapo atafikia umri wa miaka 16 (kumi na sita).

**68.2** Leseni au vibali vya mwendeshaji farasi lazima viombwe kila mwaka, huku vikiwa na jina kamili na anwani za Ofisi ya Usajili.

**68.3** Leseni na vibali vinatolewa tu kwa waendeshaji farasi wanaofaa au wanafunzi wanaofaa kwa sharti kwamba wao si wamiliki, wamiliki-kiasi au wakodishaji wa farasi yeyote wa shindano wala hawapokei zawadi kuhusiana na shindano kutoka kwa watu wengine isipokuwa Mmiliki wa farasi wanayemwendesha katika shindano hilo. Utakuwa ni ukiukaji wa Kanuni za mwendeshaji mwenye leseni kulingana na Kanuni ya 68.1 au yule anayeruhusiwa kuendesha farasi kulingana na Kanuni ya 68.4 kwenye kipindi kile cha leseni au kibali chake, kwa kuchezea karata mashindano ya farasi yanayofanywa mahali popote ulimwenguni.

**68.4** Mpaka pale ambapo mwendeshaji farasi ameshiriki katika mashindano 25 (ishirini na tano), hatapewa leseni ila atashiriki kwa idhini ya Wasimamizi wa Kuendesha Farasi kwa ada ya kuendesha farasi kama ilivyowekwa wazi katika Kanuni ya 74.1 na atapokea 10% ya marupurupu yote kulingana na Kanuni ya 74.2.

**68.5** Hakuna mtu ataendesha farasi katika shindano lolote wakati akiwa amesitishwa kwa muda na Mamlaka yoyote husika na yanayotambulika.

**68.6** Mtu ambaye hana na hajawahi kuwa na leseni ya kuendesha farasi kutoka kwa Mamlaka yoyote husika na Yanayotambulika, isipokuwa tu leseni ya kurutu na vinginevyo hajaondolewa kwenye shindano kulingana na Kanuni hizi, anaweza kutegemea ruhusa na vile vile kudhibitiwa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, na kuendesha farasi akiwa kurutu. Mwendeshaji farasi kurutu hataendesha farasi katika shindano lolote isipokuwa lile ambalo masharti yake yanamruhusu. Watu waliopewa ruhusa kuendesha farasi wakiwa kurutu hawazuiwi dhidi ya kumiliki farasi wa mashindano wala kuchezea karata shindano lolote ambalo wao hawashiriki Waendeshaji farasi kurutu wataendesha farasi bila malipo. Katika hali nyingine wataweza kuwajibikia Kanuni zinazotumika kwa waendeshaji farasi wengine.

**68.7** Farasi yeyote atakayeendeshwa kwenye shindano katika hali ya kukiuka sehemu hizi zilizotajwa kwenye Kanuni hii ataweza, kama atawekewa upingaji, kuondolewa kwenye shindano na Wasimamizi na mwendeshaji farasi pamoja na watu wanaohusika na yeye kuajiriwa kuweza kuripotiwa kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**68.8** Orodha ya watu waliopewa leseni na kuruhusiwa kuendesha farasi pamoja na uzani wao wa kuendesha farasi uliotangazwa itachapishwa kila mwaka kwenye Kalenda ya Mashindano.

**68.9** Kila mwendeshaji farasi atalipia ada iliyoshauriwa kwa minajili ya leseni au kibali chake.

## **69. Kuondolewa Shindanoni kwa Mwendeshaji Farasi**

**69.1** Mwendeshaji farasi ambaye leseni au kibali chake imeondolewa kwa misingi ya utovu wa nidhamu ndiye mtu aliyeondolewa kwenye shindano.

**69.2** Iwapo mwendeshaji farasi atakuwa mtu aliyeondolewa kwenye shindano kwa sababu nyingine yoyote basi leseni au kibali chake kitaweza kukataliwa kabisa.

## **70. Kuhifadhiwa kwa Mwendeshaji Farasi**

**70.1** Kuhifadhiwa kwa mwendeshaji farasi husitishwa kila mwisho wa msimu wa shindano la mbio za farasi.

71. Kipindi cha mikataba yote kati ya wamiliki, Watoaji Mafunzo na waendeshaji farasi kitaidhinishwa kwanza na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi na mkataba huo baadaye kusajiliwa kwenye Ofisi ya Usajili pindi tu malipo ya ada iliyoshauriwa yatakapofanywa. Hakuna mkataba ambao utamruhusu mwendeshaji farasi kushiriki kwa ada ya kiwango cha chini zaidi kuliko kile kilichowekwa wazi katika Kanuni ya 74.1.

72. Wajiri wanaohifadhi mwendeshaji farasi yuleyule watapewa kipaumbele kulingana na uzingatifu wa wale wanaohifadhiwa.

73. Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wanaweza kuwa waamuzi kati ya watu wanaodai huduma za mwendeshaji farasi yeyote na mizozo kati ya waendeshaji farasi na wajiri wao, na wanayo nguvu ya kukati'za mkataba wowote kati ya wale ambao wamesajiliwa na Mshikadau husika.

#### **74. Ada ya Mwendeshaji Farasi**

74.1 Ada ya waendeshaji farasi itaweza kuamuliwa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi baada ya muda fulani. Hakuna ada zozote za ziada zitakazotozwa.

74.2 Waendeshaji farasi wote, isipokuwa waendeshaji farasi makurutu walio na leseni na waliosajiliwa kulingana na Kanuni ya 68.6 watapokea 10% ya marupurupu yote, ya ushindi na mahali husika kutozwa na Mshikadau husika.

#### **R3. Waendeshaji Farasi Waliohifadhiwa**

R3.1 Kwa mujibu wa haki za kuhifadhiwa, kama mwendeshaji farasi amesajiliwa na amekubali kuendesha farasi aliyebainishwa katika shindano lolote na kisha pakatokea mwendeshaji farasi mbadala baada ya thibitisho la mpangilio wowote wa uendeshaji farasi, anaweza, kama hakupendezewa na uamuzi huo, kuandikisha malalamishi rasmi kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi. Kama wataamua kuwa misingi ya usawazisho huo haikueleweka, basi malipo yatalipwa tu mwendeshaji farasi aliyehusishwa mwanzo lakini si, kama itawezekana, asilimia yoyote ya malipo hayo yanayofaa kuenda kwa mwendeshaji farasi ambaye hatimaye ataendesha farasi. Mtoaji Mafunzo mhusika anayo haki ya kufanya mipangilio yake mwenyewe ya uendeshaji farasi, pamoja na kusawazisha na kubadilisha waendeshaji farasi.

R3.2 Waendeshaji farasi wanaokataa kuendesha farasi ili kuendelea kuendesha farasi wa awali (hajjalishi kama ni wa kwanza ama wa pili) huenda wasiendeshe farasi mwengine kwenye shindano hilo anayetoka kwenye vibanda tofauti vya farasi.

R3.3 Waendeshaji farasi ambao hawawezi kuendesha farasi kutoka kwenye vibanda vya mwanzo vya farasi kutokana na kutoweza kutimiza kipimo cha uzani, wanaweza kuendesha farasi kutoka katika makao tofauti kwenye shindano lilo hilo.

R3.4 Mwendeshaji farasi aliyehifadhiwa anayo haki ya kukataa kuendesha farasi ambaye anamwona kuwa hatari, lakini huenda asiweze kuendesha farasi kutoka kwenye makao tofauti kwenye shindano lilo hilo.

#### **R4. Waendeshaji Farasi Kurutu**

R4.1 Watu wanaonua kushiriki katika mbio za mashindano ya kurutu lazima wahakikishe kwamba wako katika siha njema bora na wanao uwezo wa kufanya hivyo.

**R4.2** Wasimamizi hawatakubali kisingizio cha kushindwa kuenda kwa mstari wa moja kwa moja au ukiukaji wingine wowote wa Kanuni za Mbio za Mashindano ya Farasi, huku kisingizio kikiwa kwamba mwendeshaji farasi hakuweza kudhibiti farasi wake.

## **8. VIFAA**

---

### **99. Vifaa na Matumizi Yake**

**99.1** Hakuna mwendeshaji farasi ataendesha kwenye shindano lolote isipokuwa kama ameivalia kofia ya fuvu iliyo na ruwaza iliyoidhinishwa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi na ambayo iko katika hali nzuri.

**99.2** Tandiko la farasi litajumuisha tandiko lenyewe, kamba husika, vyuma na ngozi, pamoja na mkanda wake au mshipi. Mtoaji Mafunzo anao wajibu wa hali nzuri wa tandiko hili la farasi na ufaavu wa vifaa vyote vinavyotumika (pamoja na kofia ya fuvu ya mwendeshaji farasi) inayotumika katika shindano licha ya hoja kwamba mwendeshaji farasi angependa kutumia tandiko lake binafsi la farasi.

**99.3** Kila farasi anayeshiriki katika shindano atakuwa na tandiko safi la farasi - kitambaa kilicho na nambari husika kwenye kadi ya shindano. Mwendeshaji farasi atapewa kitambaa hiki wakati wa kupimwa uzani kabla ya shindano na lazima kivaliwe ili nambari hilo liweze kuonekana waziwazi. Mwendeshaji farasi atakiweka kitambaa hicho kwenye mizani na kukijumuisha katika uzani wake, na baada tu ya kupimwa uzani kufikia mwisho wa shindano atakiwasilisha kwa Ofisa aliyepangiwa kukipokea.

**99.5** Hakuna kifaa mbadala kama hatamu au vifaa vinginevyo, vitakavyobebwa na kutumika kama mjeledi katika shindano lolote. (06/06/17)

### **TR3.2 Tandiko la Farasi na Mkanda wa Farasi**

Mwendeshaji farasi wowote anayeona kwamba mkanda wake wa farasi unahitaji kupunguzwa baada ya kuwasili kwenye sehemu ya mwanzo wa shindano anafaa, kama itawezekana, kuhurekebisha mwenyewe, lakini kama hataweza kufanya hivyo anaweza kutafuta msaada kutoka kwa Msaidizi wa Mwanzilishi.

### **TR4. Vifaa Vyenye Kasoro (30/03/16)**

**TR4.1** Endapo tandiko la farasi litateleza upande wa nyuma au mbele wakati mbio za farasi zikiendelea, Mtoaji Mafunzo na/au mwendeshaji farasi lazima waripoti tukio hilo kwa Wasimamizi na kupendekeza kile kinachohitajika ili kuepukwa tukio hilo kufanyika tena.

**TR4.2** Wakati ambapo tandiko la farasi litateleza-tena kwenye farasi yuleyule katika shindano la mbio za farasi zitakazofuata, basi kwa minajili ya usalama na uendesaji farasi unaostahili, Mtoaji Mafunzo anaweza kutozwa faini na Wasimamizi, endapo watagundua kwamba kuteleza uko kungeweza kuepukwa.

**TR4.3** Endapo kifaa chochote kingine (vikiwemo lakini si tu vishikilia miguu, hatamu, kishikilia pua, na kadhalika) kuteleza au kuvunjika wakati wa mbio za farasi, lazima mwendeshaji farasi aripoti tukio hilo kwa Wasimamizi na kuleta kifaa kile kilichokusika wakati anapotoa ripoti ili Wasimamizi waweze kukifanyia ukaguzi wa kuchuka hatua.

## **TR5. Kofia za Kuinga Fuvu, Viatu na Vifaa vya Kuinga Mwili (11/10/18)**

**TR5.1** Kofia za kuinga fuvu ambazo zimeidhinishwa na kufungwa wakati wowote, na viatu ambavyo vimeidhinishwa lazima zivaliwe, kila wakati farasi anapoendeshwa, iwe ni kwenye mbio za shindano la farasi, mafunzo, mazoezi au vinginevyo. Mtoaji Mafunzo anao wajibu kuhakikisha kwamba kofia inayokinga fuvu na kuvaliwa na mwendeshaji farasi wake iko katika hali nzuri.

**TR5.2** Kofia ya kuinga fuvu inapoanguka katika shindano, Wasimamizi watakutana baada ya shindano kuchunguza kilichosababisha kofia ya kuinga fuvu kutoka kichwani. Wasimamizi wakidhibitisha kofia ilianguka kwa sababu ya kutojali, basi huyo mwendeshaji farasi atatozwa faini kulingana na Maagizo ya Wasimamizi ya G11. (09/05/17)

**TR5.3** Zaidi ya mahitaji ya Kanuni ya 99, hakuna mwendeshaji farasi yeyote ataruhusiwa kuendesha farasi katika shindano lolote isipokuwa amevaa kifaa cha kuinga mwili kilichoidhinishwa na Wasimamizi na ambacho ni cha hali nzuri. Mtoaji Mafunzo anao wajibu wa kuhakikisha kifaa cha kuinga mwili kimevaliwa na mwanafunzi mwendeshaji farasi wake. Zaidi ya Kanuni ya 97.9, kifaa cha kuinga mwili lazima kiambatanishwe katika kupima uzani na zaidi ya Kanuni ya 97.7, uzani wa Zaidi ulioruhusiwa umeongezwa kufika kilo 3 (tatu). Kanuni ya 116 itaendelea kutumiwa kama ilivyotajwa. (10/05/19)

## **9. UKIMBIAJI WA FARASI**

---

### **102. Ukimbiaji wa Farasi**

**102.1** Kila farasi anayekimbia kwenye mbio za farasi atashiriki kutokana na manufaa yake, haijalishi kama Mmiliki wake au Mtoaji Mafunzo anashiriki pia kwa kutumia farasi mwengine kwenye shindano hilo au la.

**102.2** Mwendeshaji farasi wa kila farasi atatalia maanani masuala yote yanayoeleweka na kuruhusika kwenye shindano lote la mbio za farasi ili kuhakikisha kwamba farasi wake amepewa fursa kamilifu ya kushindana au kupata nafasi bora zaidi unaowezekana kwenye uwanja na lazima aendeshe farasi wake hadi mwisho wa shindano.

**102.3** Litakuwa ni jukumu la Mtoaji Mafunzo kuhakikisha kwamba mwendeshaji farasi amepewa maagizo tosha kuhusu farasi yeyote aliye katika utunzaji wake na kwamba hakuna Mmiliki, Mtoaji Mafunzo au Ajenti Aliyeidhinishwa atakayetoa maagizo yoyote kwa mwendeshaji farasi wa farasi yeyote ambaye, kama yatasikizwa, yangeweza au yatazuia farasi dhidi ya kushinda kwenye shindano au kupata nafasi bora zaidi inayowezekana kwenye uwanja, wao pia wataweza, mwendeshaji farasi wake au mtu yeyote mwengine kuzuia, au kujaribu kuzuia kwa njia yoyote ile farasi yeyote dhidi ya kushinda shindano au kupata nafasi bora zaidi inayowezekana.

**102.4** Mtu wowote, kwa maoni ya Wasimamizi wa Mkutano, anaweza kukiuka au kuchangia katika kukiuka sehemu yoyote ya Kanuni ya 102.1, 102.2 au 102.3 anaweza kuadhibiwa na farasi wake kuondolewa kwenye shindano.

**102.5** Mwendeshaji farasi wowote, ambaye kwa maoni ya Wasimamizi, ameendesha farasi kwa njia isiyofaa au kusababisha uingiliaji kati kwa njia hatari au isiyomakinika, atakuwa na hatia ya kosa. Hali hii haitumiki kwenye kategoria ya Uingiliaji Kati Bila Kukusudia.

## **102.6 Uendeshaji Farasi wa Hatari na Bila Kumakinika**

### **102.6.1 Uendeshaji Farasi wa Hatari**

Mwendeshaji farasi anayo hatia ya Uendesha Farasi wa Hatari kama atasababisha uingiliaji kati mbaya kwa kuingilia kati kimakusudi farasi mwengine au mwendeshaji farasi mwengine au kama ataendesha farasi kwa kiwango cha chini zaidi na kisichokubalika, na kusababisha uingiliaji kati mbaya, ambao utahatarisha usalama, na hatili maanani athari zake.

### **102.6.2 Uendeshaji Farasi Usiomakinika**

Mwendeshaji farasi anayo hatia ya Kuendesha Farasi Bila Kumakinika iwapo atashindwa kutahadhari kwa njia ya kueleweka ili kuepuka kusababisha uingiliaji kati au kusababisha uingiliaji kati kwa kufanya uamuzi mbaya au kukosa kumakinika au kama ataendesha farasi kwa njia isiyoeleweka kiasi kwamba uingiliaji kati huo hauwezi kuepukwa.

### **102.7 Uendeshaji Farasi Usiokuwa Bora**

Mwendeshaji farasi anayo hatia ya Kuendesha Farasi kwa Njia Isiyo Bora iwapo atahatarisha kimakusudi usalama wa mwendeshaji farasi mwengine au farasi mwenyewe, bila ya kusababisha uingiliaji kati.

## **102.8 Uingiliaji Kati Bila Kukusudia**

Uingiliaji Kati Bila Kukusudia unaweza kufanyika, hata kama mwendeshaji farasi atachukua tahadhari zinazoeleweka kuzuia uingiliaji kati huo au kwa hali ambazo ni zaidi ya udhibiti wa mwendeshaji farasi.

**102.9** Mwendeshaji farasi yeyote anaweza kuadhibiwa iwapo atafanyiwa uchunguzi, kwa maoni ya Wasimamizi, kama atashindwa kuendesha farasi wake hadi mwisho wa shindano.

## **103. Uingiliaji Kati, Kutumia Njia Isiyofaa na Kukimbia Ovyo Ovyo**

**103.1** Katika hali ambazo Wasimamizi wameamua kwamba mwendeshaji farasi anayo hafa ya Kuendesha Farasi kwa Hatari, Bila Makini au kwa Njia Isiyofaa, basi pamoja na adhabu iliyoshauriwa mwendeshaji farasi anaweza kurejelewa kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi ili kuweza kuchukuliwa hatua zaidi inayowezekana ya kinidhamu.

**103.2** Katika hali ambayo Mwendeshaji farasi ameendesha kwa Njia ya Hatari, farasi ataondolewa kwenye shindano.

**103.3** Katika hali zile ambazo Wasimamizi wameamua kwamba mwendeshaji farasi anayo hafa ya Kuendesha Farasi Bila Makini au kwamba tukio la Uingiliaji Kati wa Bila Kukusudia limetokea, Wasimamizi wataweza tu kutekeleza kurudisha nyuma farasi husika, kama watagundua kwamba uingiliaji kati kama huo umeboresha nafasi ya farasi huyo husika aliyesababisha uingiliaji kati huo. Kurudishwa nyuma kwa farasi kunaweza kujumuisha hata kumweka farasi huyo kuwa mwisho.

**103.4** Wasimamizi wanaweza kuulizia suala la kukimbia ovyo ovyo na kutilia maanani utendakazi wa farasi na hali nyingine zote zinazofaa kwenye vikao vya awali na kuchukua hatua mwafaka kulingana na Kanuni ya 13 kama vile watakavyoamua.

**103.5** Iwapo baada ya uchaguzi uliotajwa katika Kanuni ya 103.4 kuendesha farasi ovyo ovyo kutapatikana kuwepo kutokana na kutotegemewa kwa farasi au ukosefu wa ubora wa farasi husika, Wasimamizi wa Kikao wataweza kuweka kipindi kisichopungua siku 21 (ishirini na moja) ambacho farasi huyo atapigwa marufuku dhidi ya kushiriki katika shindano la mbio za farasi na maagizo yoyote ambayo tayari yatakuwa yamewasilishwa yatatupiliwa mbali kulingana na Kanuni ya 5.5.

**TR8. Utoaji wa Mafunzo na Uwekaji Masharf**

Pale ambapo, kwa maoni ya Wasimamizi, Mtoaji Mafunzo ameshughulikia farasi yeyote kwa nia ya kutoa mafunzo au kuweka masharf, Mtoaji Mafunzo atakuwa na hafa ya kosa. Pale ambapo Mwendeshaji farasi atapatikana kuwa amekiuka Kanuni ya 102.2 kuhusiana na utoaji mafunzo au uwekaji masharti, Mtoaji Mafunzo ataonekana kuwa na hatia ya kosa kulingana na Kanuni ya 102.3 isipokuwa kama Mtoaji Mafunzo atatosheleza Wasimamizi kwamba mwendeshaji farasi alipewa maagizo tosha na kushindwa kuyatii.

**10. UPINGAJI NA MAULIZIO**

---

**14. Upingaji na Maulizio**

**14.1** Wasimamizi wanayo nguvu kwa njia ya notisi zinazoonyeshwa kwenye ubao wa nambari au kwingineko na kwa mfumo wowote ule wa kipaza sauti kule kwenye Uwanja wa Mashindano ya Mbio za Farasi kukariri na kutangaza kwamba upingaji umeandikishwa, mada na asili ya upingaji huo na pia uamuzi wao kwa mujibu wa upingaji kama huo, au kuhusu suala lolote jingine linalohusika ndani ya mamlaka yao.

**14.2** Wasimamizi wataweza kutekeleza uchunguzi katika tukio lolote lililofanyika bila kukusudia katika shindano la mbio za farasi kati ya wakati ule ambao mwendeshaji farasi amepimwa uzani kabla ya shindano, na matokeo ya uchunguzi yatachapishwa kwenye Kalenda ijayo ya Mbio za Farasi.

**15.** Wasimamizi wanayo nguvu ya kuamua maswali yote yanayotokana kwa mujibu wa mbio za farasi kwenye kikao husika, kutegemea na rufaa kulingana na sehemu ya XXIII ya Mizozo, Upingaji, Maulizio na Rufaa.

**TR1. Maulizio**

Katika kikao, Watoaji Mafunzo, au Wasaidizi wao, walioidhinishwa wote wanahitajika kuendelea kupatikana kwenye uwanja wa mashindano mpaka pale ambapo ishara ya kupimwa uzani baada ya shindano itakapotolewa kuhusiana na shindano lolote la mbio za farasi ambalo mwendeshaji farasi wao yumo. Waendeshaji farasi vile vile wanahitajika kupatikana palepale uwanjani baada ya shindano lolote ambalo wameshiriki.

Kila wakati, Watoaji Mafunzo na waendeshaji farasi lazima waweze kupatikana katika dakika 20 (ishirini) baada ya shindano la mwisho, isipokuwa ambapo Watoaji Mafunzo na waendeshaji farasi wamejulisha Wasimamizi kwamba wanaondoka mapema. (16/07/15)



## **11. UPINGAJI: LINI NA VIPI UNAVYOTOLEWA**

---

### **127. Upingaji: Lini na Vipi Unavyotolewa**

**127.1** Iwapo kutakuwa na upingaji kwa farasi anayehusishwa katika shindano kwa muda usiopita 10:30 asubuhi kwenye siku ya shindano, Wasimamizi wanaweza kuhitaji kufuzu kwake kuweze kuthibitishwa kabla ya shindano la mbio za farasi, na endapo thibitisho kama hilo litakuwepo na kuwatoshleza basi wanaweza kumtangaza kuwa ameonolewa kwenye shindano.

**127.2** Upingaji wa kitalifa cha sehemu ya kushiriki kwenye shindano iliyoungwa rasmi lazima kufanywe kabla ya shindano.

**127.3** Upingaji wowote wa Karani wa Mizani lazima ufanywe mara moja.

**127.4** Upingaji wowote wa farasi yeyote kwa misingi ya kuvuka, kushtuka au kitendo chochote kwa upande wa mwendesha wake, au wa farasi mwenyewe kutoweza kukimbia kwenye sehemu inayofaa, au ule wa shindano kuweza kufanywa kwenye sehemu isiyofayaa, au suala jingine lolote lililofanyika kwenye shindano, au kabla ya kupimwa uzani baada ya shindano, au kwa misingi ya kwamba mwendeshaji farasi hakujiwasilisha ili kuweza kupimwa uzani baada ya shindano (Kanuni ya 118) au kwamba hakuweza kufikia uzani ambao ulipatikana alipopimwa uzani kabla ya shindano (Kanuni ya 116), vyote lazima zifanywe ndani ya dakika 5 (tano) za ule muda ambao Jaji ametangaza uamuzi wake kuhusu masuala yote husika, mradi tu kwamba Karani wa Mizani amekamilisha ule upimaji wa mizani wa baada ya shindano (tazama pia Kanuni ya 129.2). Wasimamizi wanaweza kurefusha kipindi lilichotajwa hapo juu kama wametoshaka kwamba upingaji usingeweza kutolewa ndani ya muda huo (tazama Kanuni ya 114). Hakuna upingaji kwa misingi yoyote ingine kuliko hii utaweza kusikizwa ndani ya muda huu.

**127.5** Upingaji wa misingi yoyote mingine kuliko ile iliyowekwa wazi katika Kanuni ya 127.4 utaweza kupokelewa ndani ya siku 14 (kumi na nne) kabla ya kuhitimishwa kwa kikao. Hakuna upingaji katika haya hii unaweza kusikizwa mpaka pale ambapo ishara imetolewa kulingana na Kanuni ya 114.

**127.6** Iwapo kutakuwa na udanganyifu, au taarifa isiyokuwa sahihi, hakutakuwa na kikomo katika muda wa kufanya upingaji mradi tu kwamba Wasimamizi wametoshaka kuwa hakukuwa na kucheleweshwa kusikohitajika kwa upande wa mpingaji. Upingaji kama huo hautasikizwa mpaka pale ambapo ishara imetolewa kulingana na Kanuni ya 114.

**127.7** Hakuna kitu katika Kanuni hii kitazuia operesheni wakati wowote wa Kanuni ya 6 au Kanuni ya 13.

**128.** Kila upingaji utakuwa kwa maandishi, na lazima upigwe saine na Mmiliki wa farasi husika katika shindano, Ajenti wake Aliyeidhinishwa, mwendeshaji farasi huyo, Mtoaji Mafunzo au mwajiriwa wa Mtoaji Mafunzo hayo.

**128.1** Kwenye kesi zinazopatikana kwenye Kanuni ya 127.4, lazima ziwasilishwe kwake Karani wa Mizani, isipokuwa kama upingaji huo utatolewa na Karani wa Mizani mwenyewe kulingana na Kanuni za 113 au 117.

**128.2** Katika hali nyingine zote lazima Wasimamizi wa Kuendesha Farasi waweze kuwasilishiwa kwenye Ofisi ya Usajili.

**128.3** Mpingaji ataweza, kwa wakati wa kutoa upingaji, kutuma ada iliyoshauriwa ambayo, kama kesi itaamuliwa dhidi yake, zitaachiwa Jockey Club of Kenya, isipokuwa tu kama kulikuwa na misingi mizuri na ya kueleweka kwa upingaji huo; na endapo upingaji huo utaamuliwa kuwa wa kipuzi na usiofaa, Wasimamizi watakuwa na nguvu na mamlaka ya kutoza faini mpingaji faini iliyoshauriwa.

**129.** Kila upingaji utakuwa kwa maandishi, na lazima upigwe saini na Mmiliki wa baadhi ya farasi zilizoshiriki kwenye shindano, Ajenti wake Aliyeidhinishwa, mwendeshaaji farasi wake, Mtoaji Mafunzo au mwajiriwa wa Mtoaji Mafunzo.

**129.1** Upingaji unaweza pia kutolewa bila ya kutuma kwa ada na Msimamizi au Ofisa mwenye leseni wa kikao katika wadhifa wake rasmi wa kufanya hivyo, upingaji kama huo utakuwa kwa maandishi na utapigwa saini na Msimamizi au Ofisa mwenye leseni.

**129.2** Uchunguzi utakaoitishwa na Wasimamizi katika suala lolote lililomo kwenye Kanuni ya 127.4 ndani ya muda ule ulioshauriwa na Kanuni ya 127.4 utakuwa na nguvu na athari za upingaji na Kanuni zote zinazofaa zitaweza kufanya kazi utadhania kwamba upingaji ulikuwa umeandikishwa.

**130.** Upingaji hauwezi kutupiliwa mbali bila ya idhini ya Wasimamizi au pale inapofaa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**131.** Hakuna farasi ataondolewa kwenye shindano kutokana na kosa lolote au ukiukaji wowote wa Kanuni ya ingizo, ambalo huenda lilisahihishwa kupitia kwa malipo ya faini, lakini Wasimamizi wanaweza kutoza faini, au vinginevyo kushughulikia mtu yeyote aliyesababisha makosa hayo.

**132.** Kama kulingana na Kanuni ya 103.3, nafasi mhusika ataweza kurudishwa nyuma, farasi wale wengine watachukua nafasi za mbele na kutozwa tuzo kulingana na uamuzi wa Wasimamizi.

**133.** Kutegemea na uamuzi wa upingaji, tuzo yoyote ambayo farasi aliyewasilishiwa upingaji huenda alishinda au anaweza kushinda kwenye shindano la mbio za farasi itaweza kuchukuliwa mpaka pale ambapo upingaji utaamuliwa na ada yoyote ya mashindano hayo inayoweza kulipwa na Mmiliki wa farasi mwengine itaweza kulipiwa na kushikiliwa na Mshikadau, kwa niaba ya mtu ambaye huenda alistahili kuilipia.

## **12. RUFAA NA MAULIZIO**

---

### **134. Rufaa na Maulizio**

**134.1** Mtu wowote atakayeleta upingaji wowote, au mtu wowote aliyeketwa mbele ya Wasimamizi au Wasimamizi Wanaopata Marupurupu ambaye hajafurahia uamuzi wao atastahili kukata rufaa kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi. Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wanaweza kuanzisha uchunguzi kama wanavyoruhusiwa kulingana na Kanuni 5.7, 5.8 na 5.9.

**134.2** Yule anayekata rufaa ataandikisha notisi ya rufaa kwenye Ofisi ya Usajili ndani ya siku 7 (saba), au endapo rufaa itakatwa na mwendeshaji farasi dhidi ya kusitishwa kwa muda kulingana na Kanuni ya 13.4 au 6.3.4 ndani ya saa 48 (arobaini na nne), za uamuzi kutangazwa, pamoja na kutumwa kwa ada iliyoshauriwa, ambayo itaweza kutupiliwa mbali isipokuwa kama Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wataamua kwamba kulikuwa na misingi mizuri na ya kueleweka katika rufaa hiyo.

**134.2.1** Lazima Notisi ya Rufaa iweke wazi kwa ujumla msingi wa rufaa na kupigwa saini na yule anayekata rufaa.

**134.2.2** Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wanaweza kuthibitisha au kutohibitisha uamuzi wa Wasimamizi au Wasimamizi Wanaopata Marupurupu au wanaweza kutumia nguvu zozote walizopewa kulingana na Kanuni ya 6.

**134.3** Bei zote na gharama zinazohusiana na kikao cha kukata rufaa, na fidia yoyote inayoeleweka iliyogharamika, itaweza kulipwa na mtu kama huyo, na kwa vipimo kama hivyo ambavyo Wasimamizi wa Kuendesha Farasi watakvyoelekeza.

**134.4** Hamna yeyote atawakilishwa kisheria kwenye uchunguzi wa au kukata rufaa kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**134.5** Licha ya chochote kilichomo katika Kanuni hizi, wakati ambapo rufaa imeweza kuanzishwa kikamilifu dhidi ya kusitishwa kwa muda kulikowekwa kulingana na Kanuni hizi, Wasimamizi wa Kuendesha Farasi watasitisha hali kama hiyo ya kusitishwa mpaka pale ambapo rufaa kama hiyo itakapoamuliwa.

**134.6** Hakutakuwa na rufaa yoyote kutokana na uamuzi wa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi katika hali ambazo wamekataa au wameondoa leseni ya Mtoaji Mafunzo au mwendeshaji farasi, au wakati ambapo wametangaza mtu kuwa hafai kuwa ameondolewa kwenye shindano.

## **13. BODI YA WAKURUGENZI/KAMATI YA KINIDHAMU**

---

### **135. Bodi ya Wakurugenzi/Kamati ya Kinidhamu**

**135.1** Mtu wowote aliyeletwa mbele ya Wasimamizi wa Kuendesha Farasi na ambaye leseni yake imekataliwa au ametolewa, au ambaye ametangazwa kuwa mtu aliyeondolewa kwenye shindano na wao, atastahili kukata rufaa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Jockey Club of Kenya.

**135.2** Bodi ya Wakurugenzi itajumuisha hadi wanachama tisa wa Jockey Club, mmojawapo akiwa mwenyekiti mteuliwa. Zaidi ya hayo, kutakuwa mtu wa kisheria ambaye sio lazima awe mwanachama wa Jockey Club atakayeteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi. Hakuna mwanachama wa Bodi ya Wakurugenzi anayeweza kuchukua nafasi ya Msimamizi wa Kuendesha Farasi. Kiwango kinachofaa ili rufaa yoyote kuweza kuwasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi itakuwa wanachama watatu na mtu wa kisheria.

**135.3** Yule anayekata rufaa ataandikisha notisi ya rufaa kwenye Ofisi ya Usajili ndani ya siku 7 (saba) za uamuzi wa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi linalotangazwa, pamoja na kutumwa kwa ada iliyoshauriwa, inayoweza kutupiliwa mbali isipokuwa kama Bodi ya Wakurugenzi itaamua kwa manufaa ya yule anayekata rufaa.

**135.4** Lazima notisi ya rufaa iweke waziwazi misingi ya kukata rufaa, na kupigwa saina na yule anayekata rufaa.

**135.5** Katika kutilia maanani rufaa yoyote au suala jingine linalorejelewa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na nguvu zote za Wasimamizi wa Kuendesha Farasi kama walivyopewa na Kanuni ya 6 na nguvu nyingine zozote wanazoweza kufikiria zinahitajika.

**135.6** Licha ya chochote kilichomo kwenye Kanuni hizi, wakati ambapo rufaa imeandikishwa kikamilifu dhidi ya kuondolewa kwa leseni au kuondolewa kwa kushiriki katika shindano kulikowekwa kulingana na Kanuni hizi, Bodi ya Wakurugenzi itasitisha kuondolewa kama huku kwa leseni/kuondolewa kwenye shindano mpaka pale uamuzi utakapofikiwa wa rufaa kama hiyo.

**135.7** Bei na gharama zote kuhusiana na kikao cha kukata rufaa na fidia yoyote inayoeleweka ya kugharamia inafaa kulipwa na mtu kama huyo na kwa vipimo kama hivyo ambavyo Bodi ya Wakurugenzi itaelekeza.

**135.8** Mtu wowote anayekata rufaa kwa Bodi ya Wakurugenzi anaweza kuwakilishwa kisheria.

**135.9** Hakutakuwa na kukata rufaa kokote kutokana na uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi.

#### **14. MIENENDO ISIYOFAA NA KUONDOLEWA SHINDANONI KWA WATU, PAMOJA NA KUWA NA MIENENDO ISIYO BORA**

---

**136.** Mtu wowote atakayepatikana na hatia ya mienendo mibaya au ya udanganyifu haijalishi kama hali yake inajumuisha au haijumuishi ukiukaji wa Kanuni zozote nyingine kama hizi, anaweza kutangazwa kuwa ameondolewa kwenye shindano au vinginevyo kuadhibiwa na Wasimamizi wa Shindano la Mbio za Farasi kulingana na nguvu zao kwa mujibu wa Kanuni ya 6. Bila ya mapendeleo kwa ujumla wa haya hii, kila mtu anayo hatia ya mwenendo mbaya ndani ya maana ya Kanuni hizi ambaye:

**136.1** Anaendeleza, au anajaribu kuendeleza, au kuruhusu, au kusababisha kuendelezwa au kushirikiana katika maendelezo, ya farasi mwenye kiwango chochote chenye uzito wa asili ambao hauwezi kufuatiliwa na kuonekana kuwa ulishaji wa kawaida na uliozoeleka na ambao kwa asili yake unaweza kubadilisha utendakazi wake wa kushiriki kwenye mbio za farasi wakati ule husika; au,

**136.2** Anatoa au kuonyesha, au kuahidi kwa njia ya moja kwa moja au isiyokuwa ya moja kwa moja, hongo yoyote kwa mfumo wowote kwa mtu wowote aliye na wajibu rasmi kuhusiana na farasi anayeshiriki kwenye mbio, au kwa Mtoaji Mafunzo wowote, mwendeshaji farasi, ajenti au mtu mwingine aliye na mamlaka ya, au anayeweza kufikia, uwanja wowote wa mbio za farasi; au,

**136.3** Kuwa mtu aliye na wajibu rasmi kuhusiana na shindano la mbio za farasi, au kuwa Mtoaji Mafunzo, mwendeshaji farasi, ajenti au mtu mwingine aliye na mamlaka ya, au ufikivu wa, uwanja wowote wa shindano la mbio za farasi, anayekubali au kuonyesha kukubali hongo yoyote kwa mfumo wowote; au,

**136.4** Anaingia kwa hiari au anasababisha yeye kuigizwa katika shindano lolote la mbio za farasi, au kusababisha kuanza katika shindano lolote la mbio za farasi, farasi ambaye yeye mwenyewe anajua au kuamini kwamba ameondolewa kwenye shindano; au,

**136.5** Kwa njia ya siri anapokea taarifa inayoheshimu kesi dhidi ya mtu wowote au watu waliojijhusisha ndani, au katika huduma ya mmiliki au Mtoaji Mafunzo wa farasi walio kwenye kesi, au kuheshimu farasi yeyote aliye katika mafunzo dhidi ya mtu wowote katika huduma kama hizo; au,

**136.6** Anapotosha kimakusudi au kwa kitendo chochote cha waziwazi analenga kupotosha Wasimamizi au Wasimamizi wa Kuendesha Farasi katika uchunguzi wowote; au,

**136.7** Anayo hatia ya, au anakula njama na mtu wowote mwingine kwa minajili ya kutendwa kwa, au kula njama na mtu wowote mwingine aliye na hatia ya, mwenendo wowote mbaya (au wa wizi) kuhusiana na shindano la mbio za farasi katika nchi hii au yoyote nyingine, au ameshtakiwa kwa kosa lolote la kihalifu kuhusiana na shindano la mbio za farasi katika nchi hii au nyingine yoyote; au,

**136.8** Anaingiza au kuendesha farasi katika shindano lolote la mbio za farasi kupitia kwa ufafanuzi wa uwongo na wa udanganyifu; au,

**136.9** Kitendo kingine kama hicho ambacho kitajumuisha Kanuni hizi.

**137.** Mtu wowote ambaye ameondolewa kwenye shindano ama na Jockey Club of Kenya au Mamlaka yoyote mengine thabiti na yanayotambulika ni mtu aliyeondolewa kwenye shindano kulingana na Kanuni hizi mradi tu kwamba mchakato huo wa kuondolewa kwenye shindano uendelee.

## **145. Kuchukua Hatua kwa Njia Isiyo Bora**

**145.1** Hakuna mtu atachukua hatua kwa njia ya vurugu au isiyo bora katika ardhi yoyote au makao yaliyotumika, yaliyopewa leseni au kudhibitiwa na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi na hakuna mtu atatekeleza kitendo chochote kilicho na uwezekano wa kusababisha madhara mabaya katika masilahi ya shindano la mbio za farasi nchini Kenya au kuleta sifa mbaya katika shindano la mbio za farasi nchini Kenya, haijalishi kama kitendo hicho kinaweza kujumuisha au kutojumuisha ukiukaji wa Kanuni zozote zile zinazoendelea za Shindano la Mbio za Farasi.

**145.2** Hakuna mtu ataweza, bila ya ruhusa ya Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, kwa kuhusisha shindano la mbio za farasi nchini Kenya na mtu yeyote anayejulikana kuwa ameondolewa kwenye shindano kwa kutenda kitendo chochote kilicho na uwezekano wa kusababisha madhara mabaya kwa masilahi ya mashindano ya mbio za farasi nchini Kenya au kuletea sifa mbaya shindano la mbio za farasi nchini Kenya, haijalishi kama hali hii inakiuka au haikiuki Kanuni za Shindano la Mbio za Farasi.

**145.3** Mtu wowote anayepuuza au kukataa kuhudhuria, au kutoa ithibati katika uchunguzi wowote au rufaa yoyote wakatia atakapoombwa kufanya hivyo, atakuwa amekiuka Kanuni hizi.

**145.4** Mtu wowote ambaye mwenendo wake au mapuuza yake yamesababisha, au huenda yalisababisha ukiukaji wa Kanuni hizi, anaweza kuadhibiwa.

## **15. MWENENDO KATIKA CHUMBA CHA WASIMAMIZI**

---

### **G18. Mwenendo katika Chumba cha Wasimamizi (04/10/17)**

Wasimamizi wanao wajibu kuhakikisha kwamba mashindano yote ya farasi yanakimbia kwa haki na uwazi kuambatana na Kanuni na Maagizo ya Wasimamizi. Ili kusaidia katika wajibu huu, ni lazima kila mtu anayeitwa katika Chumba cha Wasimamizi ama mtu wowote anayetaka kupeana repoti ama anayekata rufaa lazima afuate mwenendo uliofaa ndio uwezeshe wala sio kuzuia Wasimamizi katika kutekeleza wajibu wao. Mwenendo huu uwe wa upole wa lugha na tabia na usiwe wa kubishana, ukali au kihemko. Kutoweza kuzingatia kiwango hiki kwaweza kuchukuliwa na Wasimamizi kama ukiukaji wa Agizo hili na waweza kuadhibiwa ipasavyo.

## **16. VITU VILIVYOPIGWA MARUFUKU KWA WAENDESHAJI FARASI NA OFISA WOTE**

---

### **G19. Vitu Vilivyopigwa Marufuku kwa Waendeshaji Farasi na Ofisa Wote (10/02/18)**

Wasimamizi wa Kuendesha Farasi waweza, ama watakapo shauriwa na Wasimamizi katika shindano lolote, waweza amuru mtu wowote anayeendesha farasi, mtu wowote ambaye ana leseni ya kurutu, mwendesheji farasi kutoka nchi nyingine aliyehandikishwa katika mashindano chini ya Kanuni, ama ofisa wowote aliyepewa leseni na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, kupimwa kama ametumia kitu chochote kulichopigwa marufuku kulingana na mikakati iliyo katika Kiambatisho cha H. Kutofuata agizo hili kutafuatwa na adhabu kali, kama inavyoruhusiwa katika Kanuni ya 5 na ya 6.

## **17. MASHINDANO YA MIKONO NA VISIGINO**

---

### **TR9. Mashindano ya Mikono na Visigino**

**TR9.1** Katika mashindano ya 'Mikono na Visigino', lazima waendeshaji farasi wabebe mijeledi lakini HAKUNA mwendesheji farasi anaweza kumchapa farasi kwa mjeledi ama kwa mikono kwenye hatamu au kwingineko WALA hata mwendesheji farasi huyo kupunga hewani mjeledi huo. Mjeledi huo hata hivyo, unaweza kuvutwa kupitia kwa mkono mmoja hadi mwingine mara nyingi inavyohitajika.

**TR9.2** Iwapo mwendesheji farasi atautumia mjeledi kama alivyozuilwa katika TR9.1, Wasimamizi watatumia adhabu iliyoshauriwa katika Maagizo ya Wasimamizi ya G12, pale panapowezekana, mwendesheji farasi ataweza pia kutupilia mbali pointi zozote alizopata kutoka kwenye shindano.

**TR9.3** Pale ambapo mjeledi umetumika kwa njia zisizofaa, farasi yeyote anayepata ushindi au nafasi nzuri, ambayo tuzo ya pesa italipwa, ataweza kuondolewa kiotomatiki kutoka kwenye shindano na tuzo hiyo.

**TR9.4** Watoaji Mafunzo wanakubalishwa kuhusu wajibu wao wa kutoa maagizo tosha. Wasimamizi watachukulia matumizi ya mjeledi kama ukiukaji wa masharti ya shindano na kuadhibu Mtoaji Mafunzo faini iliyoshauriwa, isipokuwa tu pale ambapo farasi mwenyewe ameondolewa kwenye shindano.

## 18. KURIPOTI HALI MBALI MBALI

---

**TR10.** Kuripoti hali mbali mbali zinazoweza kuathiri au zilizoathiri kukimbia kwa farasi.

**TR10.1.1** Watoaji Mafunzo wataripoti kwa Wasimamizi chochote kinachoweza kuathiri kukimbia kwa farasi kwenye shindano. Kulingana na maumbile yake, ripoti hii itawasilishwa mapema iwezekanavyo kabla ya shindano.

**TR10.1.2** Waendeshaji farasi wataripoti kwa Wasimamizi chochote ambacho huenda kiliathiri kukimbia kwa farasi wao wakati wa shindano. Ripoti hii itatolewa mara moja baada tu ya shindano.

Ifuatayo ni mifano ambayo lazima iweze kuangaziwa katika ripoti:

1. Kuingiliwa kati wakati wa kuondoka kwenye vibanda vya farasi;
2. Kuingiliwa kati wakati wa kukimbia;
3. Kuning'inia kwa farasi;
4. Kuteleza kwa tandiko la farasi;
5. Kukataa kwa vifaa husika;
6. Kielekezi cha farasi kinachowekwa kupitia mdomoni;
7. Kupotea kwa mjeledi;
8. Kukosa kutenda jambo;
9. Farasi kupoteza kiatu;
10. Kutosafiri kamwe;
11. Kutofaa katika kukimbia husika;
12. Hana chochote cha ziada cha kutoa;
13. Kupungua - toa sababu, kama inawezekana;
14. Farasi amemaliza shindano akiwa na machungu;
15. Farasi ametokwa na damu puani;
16. Farasi amemaliza shindano akiwa mlemavu;
17. Farasi mchanga wa kike/ aliyekomaa wa kike anayepatikana kwa sasa;
18. Farasi amekabwaroho/ amesukutua/ ameumeza ulimi;
19. Virusi shukiwa au maradhi mengine.

Mkazo unatiliwa kwamba orodha hii haitoshi na kwamba hali fulani, ambazo hazijajumuishwa hapo juu na ambazo huenda zingethiri kimsingi utendakazi wa farasi, lazima pia zitiliwe maanani kwenye ripoti hiyo husika.

**TR10.2** Mtoaji Mafunzo ataweza kuripoti pia kwa Daktari wa Wanyama chochote kinachopatikana katika mamlaka haya na kuzuilia farasi kwenye Eneo la Gwaride mpaka pale ambapo Daktari wa Wanyama atakapokuwa amemchunguza. Endapo chochote kinachoweza kuwa na mwelekeo wowote na kukimbia kwa zamani au kwa siku zijazo kwa farasi kitafahamishwa kwa Mmiliki au Mtoaji Mafunzo baada ya farasi kutoka kwenye uwanja wa shindano lazima kiripotiwe haraka iwezekanavyo.

**TR10.3** Mtu wowote atakayeshindwa kutoa ripoti inayohitajika kwa mujibu wa Maagizo haya atakuwa na hatia ya kosa.

## **19. WAENDESHAJI FARASI**

---

**R1.3** Wakati ambapo Mtoaji Mafunzo anaye zaidi ya farasi mmoja kwenye shindano, kati ya farasi hawa, mmoja tu ndiye anayeweza kuendesha na mwendeshaaji farasi mtaalamu au mgeni. Agizo hili halitumiki kwenye mashindano ya mbio za farasi yaliyoorodheshwa hapa chini.

**R1.3.1** Mashindano ya mbio za farasi ya Kenya Guineas, Fillies Guineas, Kenya Derby, Kenya Oaks, Kenya St Leger, Breeding Futurity, Champagne Stakes, Sir Ali Bin Salim, Kenya Gold Cup, Stewards Cup, Jockey Club Stakes, Civil Service Gold Cup, Delamere Gold Vase & Nakuru Champion Stakes.

**R1.3.2** Waendeshaaji farasi wote waliobakizwa watakuwa huru kukubali kuwaendeshaaji farasi nje ya makao yao ya farasi waliowabakiza kama hawatadaiwa na mtu ambaye wanafaa kubaki naye, kwa mujibu wa toleo la R1.3.

### **R1.4 Wanafunzi Waendeshaaji Farasi wa Watoaji Mafunzo**

**R1.4.1** Wanafunzi wa Watoaji Mafunzo lazima wabakizwe na Mtoaji Mafunzo aliye na wajibu wa kutuma ombi la leseni au kibali chao ili waweze kuendesha farasi. Watu wanaopenda kuwahusisha waendeshaaji farasi kama hao kwenye shindano lazima wawasiliane na Mtoaji Mafunzo husika na kupata huduma zao kupitia kwa Mtoaji Mafunzo/Mwajiri.

**R1.4.2** Wasimamizi wa Kuendesha Farasi watatilia maanani na kwa umakinifu maendeleo ya wanafunzi wa Watoaji Mafunzo wa Kenya walio katika maagizo.

**R1.4.3** Endapo mwanafunzi wa Mtoaji Mafunzo ataacha ajira ya Mtoaji Mafunzo, leseni ya mwanafunzi lazima irudishwe katika Ofisi ya Usajili ikiambatana na barua inayoeleza kwa nini mwanafunzi wa Mtoaji Mafunzo anaacha ajira kati ya siku 5 (tano) ya kuacha ajira. Mtoaji Mafunzo anayetamani kujisajili kuwa mwanafunzi wa Mtoaji Mafunzo lazima awasilishe ombi jipya la leseni, na hivyo basi kutii msimbo wa mwenendo uliofapanuliwa katika Kiambatisho cha B. Kutotii hili Agizo ni hatia na atayekiuka anaweza kutozwa faini ya hadi Kshs 20,000/- (elfu ishirini). (08/02/19)

### **R2. Uchunguzi wa Kimatibabu na Siha Njema (17.01.17)**

**R2.1** Waendeshaaji farasi wote, watakapokuwa wakiomba leseni za msimu, lazima karatasi za kuomba leseni ziambatane na fomu inayotolewa ya kimatibabu ikiwa imeidhinishwa na daktari aliye hitimu.

**R2.2** Wakati wa msimu huo huo, mwendeshaaji farasi wowote anayejiruhusu kutangazwa ataonekana kuwa anajidhinisha kuwa anayo siha njema ya kuendesha farasi. Iwapo kuna tashwishi ya kiafya anafaa kushauriana na Ofisa wa Kimatibabu kabla ya shindano.

**R2.3** Hakuna mwendeshaaji farasi atashiriki kwenye shindano lolote akiwa hana siha njema au akiwa anaguza jeraha, isipokuwa mwenye jeraha amepata idhinisho awali kutoka kwa Ofisa wa Kimatibabu. Ikiwa Wasimamizi wanahitaji mwendeshaaji farasi kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, basi uchunguzi huu utakuwa wa lazima.



## **R5. Vyeti vya Kimatibabu**

Mwendeshaji farasi wowote aliyepewa leseni na Jockey Club anayepata jeraha akiendesha kwenye uwanja wa mbio za farasi na kumlazimu kulazwa hospitalini, lazima apokee, vyeti vya matibabu kutoka kwenye hospitali husika zinazoonyesha kwamba alilazwa na pia kuruhusiwa kurudi nyumbani kutoka hospitalini kwani vyote vinahitajika kwa makusudio ya bima.

## **R6. Ajali kwa Farasi na Waendeshaji Farasi**

**R6.1** Waendeshaji farasi wote wataripoti mara moja kwa Wasimamizi kuhusiana na kuanguka kwao kwote, watakapopata ajali au kuondolewa kwenye kiti cha farasi wakati wowote tangu kupanda farasi na kushuka kutoka kwenye matandiko ya farasi. Wasimamizi wanaweza kwa uamuzi wao, kutoa amri kwamba mwendeshaji farasi afanyiwe uchunguzi na Ofisa wa Kimatibabu, ambapo pendekezo lake litakuwa ndilo la mwisho.

**R6.2** Ajali zozote kwenye vikao zinazosababisha jeraha kwa mwendeshaji farasi au farasi mwenyewe itaonekana kuwa jeraha na matokeo yake yatachapishwa kwenye Kalenda ya Shindano la mbio za farasi kulingana na Kanuni ya 23.10.

## **146. Uwajibikaji**

**146.1** Si Jockey Club wala Ofisa yeyote au mwanachama yeyote wa Kilabu atahitajika kuwajibikia mtu wowote kwa kupoteza, kuharibiwa au kujeruhiwa kwa mtu huyo kutokana au kwa njia yoyote (ama ya moja kwa moja, ama isiyokuwa kwa moja kwa moja) kutokana na kuendelezwa au kutoweza kuendelezwa kwa haki yoyote, manufaa, nguvu, wajibu, au uamuzi uliowekwa kwao au kulazimishwa au kuaminika kwa njia inayoeleweka kwamba umewekewa kwao, au kulazimishwa kwao, kulingana na Kanuni hizi.

**146.2** Jockey Club hakitakubali hasara yoyote kutokana na madhara yoyote, kupoteza kokote au uchunguzi kuhusu farasi au mtu kama huyo akiwa katika makao yake kutokana na sababu yoyote ile itakayozuka, ikiwemo madhara, kupoteza au majeraha yaliyosababishwa kutokana na mapuuzo ya mwajiriwa yeyote au ajenti yeyote wa Kilabu, au Ofisa wa kikao chochote.

## **R7. Uzoefu wa Vibanda vya Farasi vya Kuanzia**

Kabla mtu wowote kuruhusiwa kuendesha farasi katika shindano la mbio za farasi lililoanzishiwa kwenye vibanda vya farasi, mtu huyo atahitajika kuwatosheleza Wasimamizi kwamba anao uzoefu na vibanda vya farasi vya kuanzia.

## **R8. Vyumba vya Kubadilishia Nguo**

Hakuna kinywaji chochote cha kulevya kinaweza kupelekwa kwenye Vyumba vya Kubadilishia Nguo vya Waendeshaji farasi.

## **R12. Mashindano ya Mbio za Farasi ya Mita 1400 na Mita 1600**

Waendeshaji farasi wataweza, katika mashindano haya ya mbio za farasi, kukimbia wakienda kwa mstari mmoja na kwenye nafasi zao zilizotengwa hadi kwenye sehemu ya kuanzia kabla ya kuchomoka hadi kwenye uwanja wa kukimbilia. Uingiliaji kati wa kuvukavuka karibu na sehemu ya mwanzo wa shindano kwenye mashindano hayo ya mbio (au mengineyo) kutakuwa ni kosa na kutavutia kupewa nidhamu ya kawaida, na

katika hali mbaya zaidi kunaweza kusababisha kuondolewa kwenye shindano.

### **R13. Waendeshaji Farasi Wasio Makini**

Mwendeshaji farasi wowote, atakayepoteza mwelekeo wake katika shindano la mbio za farasi kwa kuangazaangaza macho yake kila mahali, na kupatikana pasipofaa na farasi bila ya yeye kujua, atakuwa na hatia ya kosa la kuendesha farasi ambalo litavutia adhabu kama ilivyoshauriwa kwenye Maagizo ya Wasimamizi ya G12.

### **R14. Kumweka Farasi Katika Hali Isiyo Sawa**

Katika hali ambazo vibanda, kama vile Mnara na Sehemu ya Kumalizia shindano, vitaweza kurusha vivuli vyake kwenye uwanja wa shindano, waendeshaji farasi lazima waweze kuwadhibiti farasi wao mpaka watakaposimama. Mwendeshaji farasi wowote anayemweka farasi wake kutokuwa sawa kwa kupunga mkono au kupiga saluti kwa umati wa watu atakuwa na hatia ya kosa la kuendesha farasi, litakalovuti'a adhabu kama ilivyoshauriwa kwenye Maagizo ya Wasimamizi ya G12.

### **R16. Mijeledi**

**R16.1** Hakuna mjeledi unaweza kutumika katika shindano lolote isipokuwa ' mjeledi wa hewa' . Mwendeshaji farasi wowote asiye na mjeledi wake lazima achukue ' mjeledi wa hewa' kutoka kwa Karani wa Mizani kabla ya kuingia kwenye Eneo la Gwaride katika shindano na lazima aurudishe kwa Karani wa Mizani anaporudi kutoka kwa shindano hilo. Kama ' mjeledi wa hewa' hautapatikana katika shindano lolote, ruhusa ya kutumia mjeledi wa kawaida (usiozidi sentimita 70 [inchi 28] kwa urefu) lazima iombwe kwa Wasimamizi. (18/10/17)

**R16.2** Wasimamizi wanaweza kutoa amri kwa mwendeshaji farasi wowote atakayepatikana na hatia ya matumizi yasiyofaa ya mjeledi kuendesha farasi kwa muda uliobainishwa bila mjeledi ama kwa kutumia mjeledi mfupi zaidi ulio na vipimo kama watakavyoamuru. (17/01/17)

**R16.3** Matumizi mabaya ya farasi hayataruhusiwa. Hali yake njema na usalama wa mwendeshaji farasi ni muhimu. Mjeledi unafaa kutumika kwa usalama, masahihisho na himizo pekee. Waendeshaji farasi wote wanafaa kutilia maanani njia bora zifuatazo za kutumia mjeledi licha ya kwamba njia hizi sizo tu:

**R16.3.1** Kumwonyesha farasi mjeledi na kumpa muda wa kuitikia kabla ya kumchapa;

**R16.3.2** Kutumia mtutu wa nyuma wa mjeledi kama kumbusho kwa farasi;

**R16.3.3** Baada ya kuutumia mjeledi, kumpatia farasi muda wa kuitikia kabla ya kuhutumia tena;

**R16.3.4** Kuhakikisha kwamba mikono yako yote imo kwenye hatamu wakati unapotumia mjeledi kwenye sehemu ya chini ya mabega katika mkao ule wa sehemu ya nyuma ya mkono;

**R16.3.5** Tumia mjeledi kwa mpigo ule wa kuruka kwa farasi na karibu sana na upande wake;

**R16.3.6** Kuuzungusha mjeledi ili kumwezesha farasi kukimbia bila kuyumbayumba.

**R16.4** Wasimamizi watafikiria kuufanya uchunguzi katika hali yoyote ile ambapo mwendeshaji farasi ametumia mjeledi wake kwa njia ambayo itawasababisha kuwa na wasiwasi na kuchapisha mifano ifuatayo inayoonyesha matumizi ya mijeledi yanayoweza kuchukuliwa kwamba ni sehemu ya kuendesha farasi kusikofaa:

**R16.4.1** Kuwachapa farasi hadi kiwango cha kuwajeruhi;

**R16.4.2** Kuwachapa farasi kwa sehemu ngumu ya mjeledi kwenye sehemu ya juu ya urefu wa bega;

**R16.4.3** Kuwachapa farasi kwa haraka bila ya kutilia maanani kuruka kwa, yani, mara mbili au zaidi kwa mruko mmoja;

**R16.4.4** Kuwachapa farasi kwa nguvu za kupindukia;

**R16.4.5** Kuwachapa farasi kwa mfululizo bila ya kuwapa muda wa kuitikia;

**R16.4.6** Kumchapa farasi ambapo hakumfanyi farasi kufanya lolote;

**R16.4.7** Kuwachapa farasi ambao tayari wameshinda waziwazi;

**R16.4.8** Kuwachapa farasi hata baada ya kupita Sehemu ya Kushindia ama kumaliza shindano;

**R16.4.9** Kuwachapa farasi popote, isipokuwa kama hali za kipekee zitaitokeza, isipokuwa kwenye sehemu husika ambazo hazifai kwa mjeledi haswa sehemu ya nyuma ya mkono au sehemu ya mbele ya mkono;

**R16.4.10** Kuwachapa farasi chini kwenye upande wa mabega kwa mjeledi ukitumia mkao wa mkono wa mbele;

**R16.4.11** Kuwachapa farasi kwa nguvu za kupindukia na mara nyingi. Wakati wa kuchunguza kesi za mijeledi mingi kupindukia iliyotumika, Wasimamizi wataweza kutilia maanani masuala yote yanayofaa kama vile kuchunguza kama:

- Idadi ya mipigo ilieleweka na ilihitajika haswa kwenye kitalifa kilichotumika ukiti'lia maanani uzoefu wa farasi;
- Kuchunguza kama farasi alikuwa akiendelea kuitikia na kiwango cha nguvu kilichotumika, na
- Endapo farasi atakuwa amechapwa mara nyingi zaidi basi ndipo mtazamo mkali zaidi utakapochukuliwa dhidi ya kiwango cha nguvu kinachofaa kutumika na kinachoeleweka.

**R16.5** Mkazo unatiliwa kwamba matumizi ya mjeledi yanaweza kuchukuliwa kuwa bora au kuwa si bora katika hali fulani ambazo hazijajumuishwa hapo juu. Kwa hasa, Wasimamizi wanaweza kumuita Mtoaji Mafunzo na mwendeshaji farasi kuhusu utumizi wa mjeledi kwa farasi wa miaka miwili. (09/05/17)

**R16.6** Farasi wanaweza kufanyiwa ukaguzi na Ofisa ambaye ni Daktari wa Wanyama naye ataripoti matokeo yake kwa Wasimamizi.

## **R16.7 Majukumu ya Watoaji Mafunzo na Wamiliki**

**R16.7.1** Wanafunzi wanafaa kujifunza kuendesha farasi kwa kutumia mjeledi kabla ya kuendesha farasi adharani. Jukumu ni lake Mtoaji Mafunzo ili kuweza kumpa maagizo mwanafunzi kuhusu matumizi bora ya mjeledi kwenye mashindano. Watoaji Mafunzo wanakumbushwa kuuhusu wajibu huu na wanapewa onyo dhidi ya kuwaruhusu wanafunzi kubeba mijeledi kabla hawajapewa mafunzo bora ya namna ya kuitumia.

**R16.7.2** Watoaji Mafunzo wanao wajibu wa kutoa maagizo kwa waendeshaji farasi wao yanayojumuisha maagizo kuhusu matumizi ya mjeledi, haswa kwa farasi walio na ngozi nyembamba, na wakati wa kuwajiri wanafunzi. Wamiliki wanaochagua kutoa maagizo ya kuendesha farasi lazima wakubali wajibu sawa na huo. Kushindwa kutoa maagizo ya kutosha ama kutoa maagizo ambayo, kama yatatiliwa maanani, yanaweza ama yatasababisha ukiukaji wa maagizo haya, kunaweza kusababisha hatua ya kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya Wamiliki au Watoaji Mafunzo.

**R16.7.3** Hatua mbaya ya kinidhamu itachukuliwa dhidi ya Mtoaji Mafunzo yeyote au Mmiliki ambaye maagizo yake ni kinyume cha hitaji ya matumizi ya mjeledi kwa njia sahihi.

**R16.8** Waendeshaji farasi wote wanaotumia vibaya mjeledi watakuwa na hati'a ya kosa na kupatikana na adhabu iliyoshauriwa katika Maagizo ya Wasimamizi ya G12, ikiwemo adhabu mbaya, ambapo jeraha kwa farasi limetokea.

**R16.9** Wasimamizi wanafaa kufikiria kama wanaweza kufanya uchunguzi kama mwendeshaji farasi ametumia mjeledi wake mara 8 (nane) au zaidi kafi ya njia panda hadi sehemu ya kumaliza.

## **R17. Kukimbia na Uendeshaji Farasi: Mambo ya Kueleweka na Kuruhusika**

**R17.1** Mahitaji ya jumla kulingana na Kanuni ya 102, ni kwamba kila farasi lazima aendeshwe kwa njia ambayo mwendeshaji farasi anaweza kuonekana kuwa amefanya majaribio ya kweli ya kumfanya farasi wake kujitahidi kwa muda unaofaa, kweli na kwa uwezo wake ili kufikia nafasi/mkao bora zaidi unaowezekana kwenye uwanja wa mashindano. Haihitajiki kutumia mjeledi ili kufimiza mahitaji haya lakini mwendeshaji farasi lazima aweze kuonyesha uendeshaji wa farasi wa mikono na visigino hadi kwenye sehemu ya kumaliza shindano.

**R17.2** Mahitaji haya yanaendelea kutumika isipokuwa na pale ambapo:

- Farasi atakuwa mlemavu au kujeruhiwa.
- Farasi atakuwa 'amechoka'.
- Farasi analo tatizo, ambalo kimsingi linaathiri utendakazi wake.

**R17.3** Katika hali kama hizo, mwendeshaji farasi anafaa kuweka mbele hali njema ya farasi kwanza, ikiwemo kumsifisha yule farasi na kumshuka kama itahitajika hivyo.

## **R18. Kuamua Uingiliaji Kati**

**R18.1** Katika kufikiria kuhusu mambo mbalimbali yanayoonyesha uingiliaji kati kulingana na Kanuni ya 102, Wasimamizi wataweza kutilia maanani mifano ifuatayo, ambayo haitoshi. Aidha matukio ambapo mwendeshaji farasi anamwondoa mwendeshaji farasi mwengine kwenye laini ambayo mwendeshaji farasi huyo anastahili kuwepo unajumuisha uingiliaji kati (udhallishaji). Haihitajiki kwamba kuwe na mtagusano wa kimwili wa uingiliaji kati kama huo kufanyika.

### **R18.1.1 Uendeshaji Farasi wa Hatari**

Mifano:

1. Kujaribu kumwondoa farasi kwa lazima kutoka kwenye laini yake.
2. Kuendesha farasi mbele ya mwengine kimakusudi ili kusababisha uingiliaji kati.
3. Mwendeshaji farasi kimakusudi kujilazimisha kati ya farasi wawili.
4. Kumchapa kimakusudi farasi mwengine au mwendeshaji farasi.

### **R18.1.2 Uendeshaji Farasi bila ya Makini - Kiwango cha 3**

Mifano:

1. Kushika mwendo/kubadilisha mwelekeo ghafla au taratibu (haswa kwenye njia ya mashindano).
2. Kutekeleza mwendo fulani wa ghafla, unaosababisha uingiliaji kati huku ikiwa wazi kwamba uingiliaji kati kama huo utafanyika.
3. Waendeshaji farasi kushika mwendo/kubadilisha mwelekeo, hivyo basi kusababisha mwendeshaji farasi mwengine kuondolewa kwenye laini yake aliyonua au aliyochokua hatua ya kukukwepa.

### **R18.1.2 Uendeshaji Farasi bila ya Makini - Kiwango cha 2**

Mifano:

1. Kuendesha farasi kwa kupita mbele ya mwenzako ili kupunguza nafasi iliyopo, huku ikiwa haionekani waziwazi.
2. Kujaribu kumpita farasi yeyote ilihali hakuna nafasi ya kutosha.
3. Kushindwa kwa kipindi fulani cha muda kuchukua hatua ya kurekebisha.

### **R18.1.2 Uendeshaji Farasi bila ya Makini - Kiwango cha 1**

Mifano:

1. Farasi kumziba mwenzake bila ya mwendeshaji farasi kujaribu kurudi kwenye laini yake, ama kwa kuuvuta mjeledi wake au kama kufanya hivyo hakutoshi kwa kutumia hatamu zake.
2. Farasi kuning'inia ndani ya au mbali na mjeledi lakini mwendeshaji farasi hachukui hatua ya kutosha ya kumrudisha kwenye laini.
3. Farasi kuning'inia au kuinamia bila mwendeshaji farasi kuchukua hatua yoyote.
4. Mwendeshaji farasi kumchapa au kudhalilisha bila kujua farasi mwengine au mwendeshaji farasi mwengine lakini kudhibiti matumizi yake ya mjeledi kwa sababu ya ule ukaribu wake na farasi au mwendeshaji farasi mwengine.

### **R18.1.3 Uingiliaji Kati wa Kiajali**

Mifano:

1. Farasi kuning'inia bila ya kuonyesha onyo.
2. Farasi kuendelea kuning'inia licha ya jitihada bora zaidi za mwendeshaji farasi katika kumzuia.
3. Farasi kuondoka kwenye laini yake bila ya kutoa onyo.

### **R19. Uamuzi wa Uendeshaji Farasi Usiokuwa Bora**

Katika kutilia maanani matukio ya Uendeshaji Farasi Usiokuwa Bora kulingana na Kanuni ya 108, Wasimamizi wataweza kutilia maanani mifano ifuatayo, ambayo pia haitoshi:

1. Mwendeshaji farasi anamchapa kimakusudi farasi mwengine au mwendeshaji farasi mwengine.
2. Mwendeshaji farasi anajaribu kimakusudi kuingilia kati farasi mwengine au kumchapa farasi mwengine au mwendeshaji farasi binafsi kwa mjeledi.
3. Mwendeshaji farasi anaendesha farasi kwa hatari lakini hasababishi uingiliaji kati mbaya.

## **20. KIAMBATISHO CHA B, MSIMBO WA MWENENDO**

---

### **Jumla**

3. Hakuna Mtoaji Mafunzo ataajiri mtu wowote mwenye leseni ambaye alikuwa ameajiriwa na Mtoaji Mafunzo mwingine bila ya kumjulisha na kupata majibu. Zaidi ya hayo, ni lazima kuwe na makubaliano yaliyoandikwa yanaoleleza vile Mtoaji Mafunzo wa kwanza atalipwa gharama aliyotumia kupata bima na leseni ya mtu huyo. (08/02/19)

### **Waendeshaji Farasi**

6. Watoaji Mafunzo lazima watii Kanuni ya 71 Kuidhinishwa na Kusajili kwa Mikataba.
7. Pale ambapo Mtoaji Mafunzo atabakisha mwendeshaji farasi, Mtoaji Mafunzo lazima afahamishe Ofisi ya Usajili ndani ya siku 5 (tano) za kuachiliwa kwa mwendeshaji farasi huyo kutoka kwenye mpangilio ule wa kumbakiza kwenye msimu husika.

### **Wanafunzi Waendeshaji Farasi wa Watoaji Mafunzo**

8. Lazima Watoaji Mafunzo watii Agizo la Wasimamizi la R1.4.1 Kubakiza Wanafunzi wa Watoaji Mafunzo.
9. Pale ambapo Mtoaji Mafunzo anasita kuajiri mwendeshaji farasi mwanafunzi, notisi ya maandishi, zikiwemo sababu za kusitishwa kwake, lazima itolewe kwa Ofisi ya Usajili ndani ya siku 5 (tano) za kusitishwa kwake.

### **Majeraha**

10. [Kama ilivyoandikwa katika sehemu 2 hapo juu,] Ni wajibu wa Mtoaji Mafunzo kuwa na jukumu la kuwajali maslahi kuhusu majeraha ya kazi na ya kuendesha farasi katika Uwanja wa Ngong. Watoaji Mafunzo kwa hivyo lazima wachukue bima itakayoshugulikia gharama ya matibabu vilivyo kwa wafanyikazi wao na waendeshaji farasi wake. Kwa hivyo, JCK haitoi bima balada ya matibabu. (24/10/19)
11. Endapo mwendeshaji farasi atajeruhiwa akiwa kwenye farasi wa Mtoaji Mafunzo mwengine, bado ni jukumu la mwajiri wa mwendeshaji farasi huyo kuweza kushughulikia gharama hizi.
12. Wakati wote ule jeraha linapotokea ambalo linao uwezekano wa kuchukua zaidi ya mwezi 1 (moja) ili kupata nafuu, Mtoaji Mafunzo atawasilisha ripoti ya maendeleo kufikia mwisho wa kila mwezi katika Ofisi ya Usajili.

**21. KIAMBATISHO CHA H, VITU VILIVYOPIGWA MARUFUKU (01/02/18)****TAFADHALI ANGALIA MSEMO WA KIINGEREZA, BS1-BS7****22. ADHABU NA POINTI ZA MAKOSA YA KUENDESHA FARASI****G12. Adhabu na Pointi za Makosa ya Kuendesha Farasi**

<b>Kosa</b>	<b>Kusitishwa (Idadi ya Vikao)</b>	<b>Pointi</b>
Kuingia kibanda kisichofaa [28.14]	0	1
>Uzani uliozidi wa kilo 2 bila ruhusa [97.8]	0	2
Kuendesha Farasi kwa Hatari [102.6.1&R18. 1.1]	4	4
Kuendesha Farasi bila Makini [102.6.2 & 18.1.2] - Kiwango cha 3	2	3
Kuendesha Farasi bila Makini [102.6.2& 18.1.2] - Kiwango cha 2	1	3
Kuendesha Farasi bila Makini [102.6.2 & 18.1.2] - Kiwango cha 1	0	3
Kuendesha Farasi kwa Njia Isiyo Bora [102.7]	4	4
Kushindwa kuendesha farasi kwa manufaa yake bila kupoteza nafasi bora [102 & TR8]	0	4
Kushindwa kuendesha farasi kwa manufaa yake na kupoteza nafasi bora [102 & TR8]	1	4
Kushindwa kutia jitihada kwa wakati unaofaa, wa kweli na zinazostahili [R17]	1	4
Kushindwa kuendesha farasi kwa kufuata maagizo [102]	1	3
Kupimwa uzani baada ya shindano > kilo 1 zaidi ya uzani kamili [116.1]	0	2
Kupimwa uzani baada ya shindano < kilo 0.5 chi ni ya uzani sahihi [116.2]	0	3
Kushindwa kupimwa uzani baada ya shindano [118]	0	2
Mwendeshaji farasi hapatikani mbele ya Wasimamizi baada ya shindano [TR1]	0	2
Kushindwa kuripoti hali zinazoathiri kukimbia kwa farasi [TR10]	0	2
Matumizi ya Mjeledi kwenye Shindano la kutumia Mikono na Visigino [TR9]	0	3
Kumfanya farasi kutokuwa sawa na/au kuangazaangaza macho [R14/R13]	0	2
Matumizi mabaya ya Mjeledi + Jeraha kwa Farasi [R16]	2	4
Matumizi mabaya ya Mjeledi [R16]	0	4
Kushindwa kubakia kwenye laini yako katika 1600 &1400 [R12]	0	2
Utumiaji mabaya wa kiwanja [T8]	0	4



1. Adhabu itatumika kwa kila kosa lililofanywa (yani hakuna tahadhari itakayotumika).
2. Pindi afikishapo pointi 10 (kumi), mwendeshaji farasi ataadhibiwa kwa kusidshwa kwenye vikao 2.
3. Pindi afikishapo pointi 20 (ishirini), mwendeshaji farasi ataadhibiwa kwa kusidshwa kwenye vikao 4.
4. Pointi za adhabu zinaweza kutupiliwa mbali pindi kosa husika litazidi miezi 12 (kumi na mbili). Hata hivyo pointi zilizotumika kwenye sehemu ya 2 hapo juu, zitaweza kutumika tena kwa kusudio la kupiga hesabu za kiwango cha juu zaidi katika pointi ya 3 hapo juu.
5. Pale ambapo tukio linajumuisha zaidi ya kosa moja, adhabu na hoja za kila kosa zitatumika.

## **ADA NA MATOLEO YALIYOSHAURIWA**

### **G10. Ada na Matoleo Yaliyoshauriwa**

**KSHS**

- |  |          |
|--|----------|
| 1. Ada za kutumwa bila ya upingaji [128]   | 1,000/-  |
| 2. Ada za kutumwa kwa minajili ya kukata rufaa kwa Wasimamizi wa Shindano la Mbio za Farasi [98.2 & 134] | 5,000/-  |
| 3. Ada za kutumwa kwa minajili ya kukata kwa Bodi ya Wakurugenzi [135]                                   | 10,000/- |

## **FAINI ZILIZOSHAURIWA**

### **G11. Faini Zilizoshauriwa**

- |  |          |
|--|----------|
| 1. Faini ya kiwango cha juu zaidi kwa ukiukaji wa Kanuni [6.3]                   | 50,000/- |
| 2. Faini ya kiwango cha juu zaidi kwa ukiukaji wa Kanuni [13.2]                  | 25,000/- |
| 10. Kushindwa kutangaza uzani tofauti na ule wa Kadi ya Shindano [94] (14/08/14) | 3,000/-  |
| 12. (a) Kutoingia kwenye Eneo la Gwaride kwa wakati unaofaa [100.2]              | 1,000/-  |
| (b) Kutoka kwenye Gwaride mapema bila ruhusa ya Wasimamizi [100.5] (04/05/16)    | 1,000/-  |
| 13. Kutoa upingaji wa kipuzi au usiofaa [128]                                    | 5,000/-  |
| 17. (a) Kutovaa kofia za kuingia fuvu zilizoidhinishwa [TR5.1]                   | 1,000/-  |
| (b) Kofia za kuingia fuvu kuanguka wakati wa shindano [TR5.2] (09/05/17)         | 2,000/-  |
| 18. Utovu mwingine wa nidhamu wakati wa Kuanza [28.14] (31/12/14)                | 1,000/-  |

## **23. WASIMAMIZI WA KUENDESHA FARASI: NGUVU NA HATUA ZA KINIDHAMU**

**6.2** Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wanayo mamlaka kama sababu nzuri itaonyeshwa au wakati ambapo mtu wowote ametenda ukiukaji wowote wa Kanuni za Mashindano ya Mbio za Farasi katika kuondoa au kusitisha kwa muda leseni au kibali chake.

**6.3** Wakati mtu wowote ametenda ukiukaji wowote wa Kanuni za Mashindano ya Mbio za Farasi, Wasimamizi wa Kuendesha Farasi wanayo mamlaka katika uamuzi wao kumtoa mtu kama huyo adhabu moja au zaidi kati ya zifuatazo:

**6.3.1** Faini isiyozidi Kshs. 50,000/- (elfu hamsini);

**6.3.2** Kusitisha kwa muda mtu wowote dhidi ya kuendesha farasi kwa mikutano isiyozidi 6 (sita) ambapo mashindano haya haswa hufanyika, mikutano kama hiyo itakuwa imefuatana;

**6.3.3** Ili kutangaza kuwa mtu huyo ameondolewa kwenye shindano;

**6.3.4** Adhabu yoyote nyingine kama ilivyoshauriwa kupitia kwa maelekezi kulingana na Kanuni ya 5.13.

**6.4** Mamlaka yanayotolewa na Kanuni hii hayafai kuonekana kwa njia yoyote ile au kwa tukio lolote lile kwamba yamewekewa mipaka au hayajajumuishwa kwa sababu ya pointi kwamba baadhi ya Kanuni zinatumika huku nyingine hazitumiki katika kushauri adhabu ya ukiukaji wake.

## **24. WASIMAMIZI: NGUVU NA HATUA ZA KINIDHAMU**

---

**13.1** Wasimamizi wanayo nguvu ya kuchunguza, kusimamia, kudhibiti, kuwa na ufahamu wa na kuamua kuhusu mwenendo wa Ofisa wote, Wamiliki, Watoaji Mafunzo, walezi wa waendeshaji farasi, watu wanaoshughulikia farasi, na watu wanaotembelea sehemu husika katika uwanja wa mbio za farasi au sehemu nyingine zinazotumika kwa makusudio ya kikao.

**13.2** Wakati ambapo katika maoni ya Wasimamizi, mtu wowote ametenda ukiukaji wowote wa Kanuni za Mashindano ya Mbio za Farasi, basi watu hao wanayo mamlaka katika uamuzi wao kumwekea mtu kama huyo faini iliyoshauriwa, au iwapo faini hiyo haijashauriwa, faini isiyozidi Kshs. 25,000/- (elfu ishirini na tano). Mamlaka haya na uamuzi huu hautumiki katika adhabu zilizoshauriwa kutokana na makosa ya mashindano ya uendeshaji farasi kulingana na Maagizo ya Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**13.3** Wakati ambao, kwa maoni ya Wasimamizi, kunayo shaka inayoeleweka kwamba mtu wowote ametekeleza ukiukaji wa Kanuni za Mashindano ya Mbio za Farasi ambapo kwa maoni yao ukiukaji huu unahitaji kutiliwa maanani na Wasimamizi wa Kuendesha Farasi, wanayo nguvu katika uamuzi wao kuweza kuripoti suala hili kwa Wasimamizi wa Kuendesha Farasi.

**13.4** Kusitishwa kokote kwa muda dhidi ya kuendesha farasi kutakakotekelezwa na Wasimamizi kulingana na Maagizo ya Wasimamizi wa Kuendesha Farasi kutatumika kwenye vikao ambavyo mbio hizi za farasi kwa hakika hufanyikia, vikao kama hivyo vitafuatana na kutekelezwa kuanzia siku ya kwanza baada ya kosa hilo kutekelezwa, isipokuwa kama kutakuwa na rufaa (tazama Kanuni ya 134.5).

## **25. MATUMIZI YA UWANJA WA MAZOEZI YA FARASI, PAMOJA NA MATUMIZI MABAYA YA UWANJA WA MBIO ZA FARASI**

---

### **TR11. Matumizi ya Uwanja wa Mazoezi**

**TR11.1** Ili kuboresha usalama na nidhamu, jezi zenye rangi tofauti zinatumika kwa matumizi ya Uwanja wa Mazoezi ya farasi kama ifuatavyo:

- Kijani ni rangi inayoonyesha ‘ kazi yenye kasi ya haraka’
- Chungwa ni rangi inayoonyesha ‘ kuruka kulikodhibitiwa kwenye mzunguko wote’
- Nyekundu ni rangi inayoonyesha ‘ kazi yenye kasi inayotofautiana na ambayo haihitajiki kuwa sawa kwenye mzunguko wote’

Jezi hizi lazima zivaliwe na waendeshaji farasi wote na sheria lazima iwe kwamba rangi nyekundu inapatia nafasi rangi ya chungwa na ambayo inapatia nafasi rangi ya kijani. Hata hivyo, Watoaji Mafunzo wanafaa kupangilia farasi wao kwa njia bora iwezekanayo ili kuhakikisha kwamba haja ya kupatia nafasi imepunguzwa kwa kiwango kidogo zaidi.

Wakati ambapo Uwanja wa Mazoezi wa Changarawe unatumika, basi jezi za kijani na chungwa tu ndizo zinazofaa kuvaliwa, na hakuna kupishana kunaruhusiwa, hata kama kufanya hivyo kunatatiza kazi inayoendelea nyuma ya farasi husika.

**TR11.2** Farasi wasiozidi 3 (tatu) kwa kila wakati wanafaa kufanya kazi pamoja kwenye Uwanja wa Mazoezi. Aidha, kila mwendeshaji farasi atakagua kwamba Uwanja wa Mazoezi farasi uko wazi zaidi kule mbele ili kazi yao ya mafunzo isiweze kutatizwa kabla ya kuanza. Kufikia wakati ule ambao farasi amefikia sehemu iliyo mkabala wa ile ya Kuanzia Mbio za 2060m, lazima farasi apunguze mwendo ili uwe wa polepole. Hakuna farasi anaweza kuvuka barabara ya magari huku akitembea. Hakuna farasi ataongozwa upande fulani au kufanyizwa kazi ya haraka zaidi kwa misingi yoyote ile isipokuwa ndani ya mipaka iliyotengwa kwa Mazoezi. Hakuna farasi ataruhusiwa kuingia au kushiriki kwa Mazoezi kati ya 6:00 jioni na 6:00 asubuhi.

**TR11.3** Hakuna farasi anaruhusiwa kuongozwa upande mmoja kwenye barabara zile mbili zinazolingilana kutoka kwenye maegesho ya gari nyuma ya huduma za JCK hadi kwenye njia ile panda na, vile vile, hakuna farasi ataruhusiwa kuongozwa kwenye upande ule wa barabara inayounganisha njia ya magari kupita kandokando ya sehemu ya mbele ya watu kukalia wanaposhuhudia shindano la mbio za farasi hadi kwenye njia panda.

**TR11.4** Mtoaji Mafunzo anaweza kuadhibiwa na Wasimamizi wa Mbio za Farasi au Msimamizi Anayepata Marupurupu au mtu wowote aliyeidhinishwa kwa ukiukaji wowote wa agizo hili na mwendeshaji farasi anayefanya kazi bila ya leseni au mwendeshaji farasi aliye na leseni. Waendeshaji farasi walio na leseni wanaweza, hata hivyo, kuadhibiwa kwa njia ya moja kwa moja.

## **T8. Matumizi Mabaya ya Uwanja wa Shindano la Mbio za Farasi**

Mtoaji Mafunzo wa farasi yeyote atakayepatikana akiendesha farasi kwenye Uwanja wa Shindano la Mbio za Farasi bila ya ruhusa, atakuwa na hatia ya kosa na atatozwa faini ya Kshs. 50,000/- (elfu hamsini) kwa kila farasi na farasi yule mmoja au farasi wale wengi wanaohusika watazuiliwa dhidi ya kushiriki kwenye mbio za farasi kwa vikao vitano vya mashindano vinavyofuatana. Aidha, joki yeyote au joki mwanafunzi wa Mtoaji Mafunzo aliyehusika katika ukiukaji wa Agizo hili ataweza kuadhibiwa kiwango kidogo zaidi cha pointi 4 (nne).

	<b>English Source Term</b>	<b>Swahili Target Term</b>
1	All Weight	Uzani Wote
2	Allowances	Kutolewa uzito
3	Amateur	Kurutu
4	Appeals and Enquires	Rufaa na Maulizio
5	Appendix	Kiambatisho
6	Apprentice	Mwanafunzi Mwendeshaji Farasi wa Mtoaji Mafunzo
7	Apprentices	Wanafunzi Waendeshaji Farasi wa Watoaji Mafunzo
8	Amateur	Kurutu
9	Assistant Starter	Mwanzilishi Msaidizi
10	Attendance	Mahudhurio
11	To authorize	Idhinisha
12	Blinker	Kizuia macho
13	Board of Directors	Bodi ya Wakurugenzi
14	Bridle	Hatamu
15	Choke	Sakama/Kaba roho
16	Clerk of the Scales	Karani wa Mizani
17	Code of Conduct	Msimbo wa Mwenendo
18	Condition	Masharti
19	Conduct	Mwenendo
20	Conduct at Start	Mwenendo Mwanzoni
21	To declare	Tangaza
22	Declared Riders	Waendeshaji Farasi Waliotangazwa
23	Declaration	Tangazo
24	Deposits	Arbuni/Uwekaji Pesa
25	Determining	Kuamua
26	Directions	Maelekezo
27	Disciplinary Committee	Kamati ya Kinidhamu
28	Disqualify	Ondoa kwenye shindano
29	Distance	Kitalifa
30	Dressing Room	Chumba cha Kubadilishia Nguo

31	Employee	Mwajiriwa
32	Even number	Nambari shufwa
33	Fitness	Siha njema
34	Girths	Mkanda wa farasi
35	To gurgle	Sukutua
36	Handbook	Kijitabu cha Maelezo
37	Heels	Visigino
38	Horse	Farasi
39	Horse Handler	Mlezi wa Farasi
40	Instructions	Maagizo
41	Jockey/Rider	Mwendeshaji Farasi/Joki
42	Jockeys/Riders	Waendeshaji farasi/Majoki
43	Judge	Jaji
44	Lead	Ongoza
45	Level	Kiwango
46	Loading promptly	Uingizaji farasi kwa haraka
47	Mounting	Kupanda
48	Objection	Upingaji
49	Objector	Mpingaji
50	Odd number	Nambari witiwi
51	Offence	Hatia
52	Order	Amri
53	Parade Ring	Eneo la Gwaride
54	Penalty	Adhabu
55	Permit	Kibali
56	Prescribed Fines	Faini Zilizoshauriwa
57	Race	Shindano
58	Reasonable distance	Kitalifa cha kueleweka
59	Recommendation	Pendekezo
60	Registry Office	Ofisi ya Usajili
61	Rule(s)/Regulation(s)	Kanuni

62	Riders' Allowances	Kuondolewa Uzito kwa Waendeshaji Farasi
63	Rings	Pete/Maeneo
64	Saddle	Tandiko la farasi
65	To saddle	Weka matandiko kwenye farasi
66	Schooling and Conditioning	Utoaji wa Mafunzo
67	Silver Ring	Eneo la Fedha
68	Skull	Fuvu
69	Skull caps	Kofia ya kuinga fuvu
70	Stakeholder	Mshikadau
71	Starter	Mwanzilishi
72	Starting	Kuanza
73	Starting Post	Sehemu ya Kuanzia
74	Starting Stalls	Vibanda vya Farasi vya Kuanzia
75	Starts	Mwanzo
76	Steward/Stewards	Msimamizi/Wasimamizi
77	Stewards of Racing	Wasimamizi wa Kuendesha Farasi
78	Stipendiary Steward	Msimamizi Anayepata Marupurupu
79	Stride	Kuruka
80	Suspension	Kusitisha kwa muda
81	Syces	Walezi wa farasi
82	Tower	Mnara
83	Trainer	Mtoaji Mafunzo
84	Unruly horse	Farasi gaidi
85	Veterinary Officer	Daktari wa Wanyama
86	Weighing In	Kupima Uzani Baada ya Shindano
87	Weighing Out	Kupima Uzani Kabla ya Shindano
88	Whip	Mjeledi
89	Winning Post	Sehemu ya Kumalizia